

NI NANI HUYU?

 . . . Bwana, na ma—mambo ambayo ameahidi. Na kila ahadi ambayo amefanya Yeye ni ya kweli. Nasi tunautazamia ule wakati wa kuonekana Kwake. Nasi tunapoiona hiyo Siku ikikaribia, saa hiyo ikija, inatufanya kutaka kujichunguza, kutoa hesabu ya nafsi zetu na kuona tu mahali tunaposimama.

² Nilikuwa tu nikisikia, nilipokuja uani huko nje, rafiki yangu mwema pale, kwamba rafiki msiri wangu yuko karibu kufa, kwa kansa. Nami hakika ninalitaka kanisa kumwombea Ndugu Rogers. Naye ni. . . Ninataka kushuka juma hili kwenda kumwona. Yeye anaishi katika mji wa yapata maili thelathini na tano, arobaini chini ya hapa, Milltown, Indiana. Nami ninataka kushuka kwenda kumwona. Yeye ni askari mstaafu wa Vita vya Kwanza vya Dunia. Naye alifanyiwa upasuaji hivi majuzi, nao madaktari wakamshona tu kwa sababu walisema, “Hakuna haja ya kujaribu kufanya upasuaji. Alikuwa yuafa.” Naye ndio kwanza ajue hilo, ninaamini, Ijumaa ama Jumamosi, mojawapo, ndio kwanza ajue kwamba alikuwa na kansa.

³ Ila jambo moja kuu lilitukia. Yeye alisema, “Mle chumbani,” hapo alipoenda ho—hospitalini, ya kwamba, “kulikuwako na upinde wa mvua uliokuja pembeni.” Naye akasimama, akauangalia kwa muda fulani. Na hiyo ilikuwa ni ishara ya Mungu ya agano. Hakika, upinde wa mvua, sikuzote unawakilisha agano.

⁴ Mungu hutimiza maagano Yake. Yeye hufanya ahadi Yake. Nami na wewe tunaweza kufanya moja na inatubidi kuivunja, kwa sababu sisi—sisi hatujui kabisa yale kesho inayoshikilia. Bali Mungu hawezi kufanya moja, na kuivunja, kwa sababu Yeye anajua yale kesho inayoshikilia. Mnaona? Yeye anajua yote kuhusu shida zetu na mambo yalivyo. Naye anajua yote ambayo yangukwako, kabla hayajakuwako. Kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, Yeye alijua ni yupi hasa angekuwako na ni nani asingekuwako.

⁵ Nayo si ni faraja, baada ya sisi kuwa na mazungumzo haya makali mno kutoka kwa huyu Mrusi, Khrushchev, na—na hao mbalimbali? Na matamshi ambayo wametoa, ambayo yanasema, “Ma—mabanda ya mabomu yako tayari. Wangeweza kuuangamiza ulimwengu katika dakika moja tu.” Mnaona? Na kitu chochote tu, wana—wanabonyeza tu kitufe na ni hayo tu. Ila kuangalia katika kurasa za Biblia hii na kuona, lakini, kabla hilo halijaweza kutukia kamwe, Kanisa limeenda Nyumbani. Loo, ni hisia ya jinsi gani, mnaona, ni faraja jinsi gani kujua hayo kamwe hayatatugusa. Hiyo ni kweli. Tutaninii. . . Kamwe hayatatugusa. Sisi ni salama tu iwezekanavyo. Na kujua ya kwamba hapo

si mahali tu pa kujificha ambapo serikali imetutengenezea. Ni mahali pa kujificha alipo napo Mungu! . . . ? . . . Nasi tunaweza kuwa na uhakika kwamba ni pakamilifu tu pawezavyo kuwa.

⁶ Kote katika nyakati, Mungu ametoa ahadi, na kupitia kwa ahadi hizi Yeye sikuzote amezitimiza. Na kwangu mimi, si—sioni lolote lililosalia ila kule kunyakuliwa kwa haraka kwa Kanisa. Ninayaona hayo makundi madogo kote kote, yakijitahidi sana; waaminifu, wakishikilia.

⁷ Na juma lililopita, mnajua yaliyotukia huko Israeli, ile ishara ya mwisho.

⁸ Israeli ilifanyika taifa mwaka wa 1947, kwenye usiku ule ule Malaika wa Bwana aliponizuru. Hapo aliponijia saa sita, ilikuwa ni aduhuri wakati walipotia sahihi ule mkataba wa amani pamoja na ulimwengu, Shirikisho la Mataifa, na kadhalika, nchi za ng'ambo.

⁹ Lakini juma lililopita walipata fedha yao wenyewe. Wao ni . . . Wana pesa za kawaida za Kiyahudi wanazotumia sasa.

¹⁰ Wala si—sioni lolote lililosalia hata kidogo, kulingana na Maandiko. Hakika, huenda . . . mambo mengi, labda, Bwana hajanijalia kujua. Bali sioni lolote lililosalia ila kule Kuja kwa Bwana. Na, loo, jinsi ninavyopenda tu kujichunguza. Nawe ukianza kusoma magazeti na kusikiliza matangazo ya habari, basi yanakupa wasiwasi kweli. Ndipo basi unaketi chini na kuwazia, “Kabla halijaweza kutukia, sisi tumeenda Nyumbani.”

¹¹ Kamwe hakutakuwako na mtu mzee kwenye Nchi hiyo. Wazieni tu, sisi wazee tutabadilishwa wakati huo, nasi tutakuwa vijana. Kamwe hakuwezi kuwako na maradhi kule; kamwe hakuna mauti. Hakuwezi kuwako na huzuni, majonzi, wala chochote wakati huo, wakati tumeyavuka hayo.

¹² Ningetaka tu kuuliza hili. Vipi kama, asubuhi ya leo, mtu fulani angeweza kuingia mlangoni na kusema, “Vema, ndio kwanza nipate kitu, ambacho kimethibitishwa kweli kisayansi. Na hicho ni, ya kwamba, kuna meli inayokuja hapa, kupitia hewani, katika dakika chache tu. Na kila mmoja wenu, anayetaka kuingia, anaweza kuingia. Nayo inaenda kwenye nchi ambayo ndio kwanza nimerudi. Nilikuwa mzee, umri wa miaka tisini”? Naye yule pale, katika upeo hasa wa ujana, mwajua, na kusema, “Ng'ambo tu kule, mara tu ukishuka ng'ambo ile, papo hapo unarudi kijana. Nami nilikutana na watu ambao wamekuwa huko kwa mamilioni ya miaka, nao walionekana tu vile vile.”

Ningesema, “Ndugu, nitengenezee tu nafasi, mimi naja.”

¹³ Nafikiri hivyo ndivyo sisi sote tunavyojisikia. Nanyi mnajua hiyo si hadithi tu. Hiyo ni kweli. Nayo ile Meli ya kale ya Sayuni itashuka kupitia hewani, moja ya siku hizi, na kuwabeba

watakatifu, na kuvuka. Twende tu chini ya beramu, ule msalaba, ndipo basi tuko Nyumbani. Loo, huo wakati mzuri sana!

¹⁴ Kwa hiyo nafikiri, leo hii, na hata kuna mateso mengi ya mwenye haki, bali Mungu humkomboa kutoka kwa hayo yote. Nami nina furaha ya kwamba tumeondoa wasiwasi katika ahadi hii kuu.

¹⁵ Ninamshukuru Mungu sana, kwa neema Yake, iliyomwita Ndugu Junior Jackson, kama tunavyomjua hapa. Niliwasikia wageni wakishuhudia dakika chache zilizopita, wakiisha kuja kwa ajili ya ibada ya uponyaji usiku wa leo. Na mimi—mimi ninashukuru sana kwamba Mungu alimwokoia Ndugu Jackson. Ibilisi alikaribia sana kumwua, wakati mmoja. Lakini Mungu alikuwa na kazi kwa ajili yake kufanya, kwa hiyo akayaokoa maisha yake. Na hiyo ndiyo sababu kusanyiko hili, kanisa dogo linalosimama hapa leo hii, ni kwa ajili ya neema ya Mungu. Junie amekuwa rafiki msiri wangu sana, mwaminifu awezavyo kuwa, kwa hii Huduma. Nami ninaomba ya kwamba Mungu atawabariki ninyi watu, hili kusanyiko hapa, na atawazidisha mpaka kanisa hili halitaweza kuwashikilia watu.

¹⁶ Nalo linanifurahisha kuingia kwenye kanisa dogo kama hili, ambapo tunaweza tu kukusanyika pamoja kwa karibu. Nimekuwa na majaliwa, kwa neema ya Mungu, kuzungumzia makusanyiko ambayo ni makubwa zaidi; bali sisemi hili, kwamba mimi—kwamba niliyafurahia zaidi. Kwa sababu, mikutano iliyobora zaidi niliyopata kuwa nayo ilikuwa ni wakati tulipokuwa na hata mikutano midogo ya nyumbani. Ambako tunanini tu... Ningejitwalia kiti na kwenda pembeni, na kuruka na kwenye kiti. Na kuwa tu na wakati mzuri sana wa ushirika, ambapo watakatifu wanaweza kukutanika pamoja. “Na popote wawili au watatu wanapokusanyika katika Jina Langu, nitakuwa katikati yao.” Hiyo ndiyo ahadi. Haijalishi ukubwa wa kanisa, Mungu aliahidi kukutana nasi. Naye atafanya hivyo.

¹⁷ Sasa, ninaamini wao... Ndugu Jackson alikuwa akiniambia ya kwamba walikuwa wakitarajia, usiku wa leo, kuwa na ibada ya uponyaji kanisani. Nami nikamwambia ningekuja pia na labda nilizungumzie kusanyiko kwa dakika chache, baada ya shule yake ya Jumapili asubuhi ya leo, na kwa namna fulani nipate kujua hisia za watu. Ndipo nikamsikia mtu fulani akishuhudia ya kwamba walikuwa wamekuja kwa ajili ya uponyaji. Nami nadhani kuna wengi, usiku wa leo, wa kuombewa.

¹⁸ Je, mlikuwa mkitarajia ibada ya kuwaleta watu huku na kuwatia mafuta, kuwaombea, ama u—u—utambuzi wa Roho Mtakatifu wa kutafuta kujua kuna shida gani? Na, mnaona, mambo hayo sina budi kujiandaa kwa ajili yake, pasipo kula, kumngojea Bwana, kadhalika, kwa sababu Shetani sikuzote yu

karibu, kutega mtego, wakati wowote tu kukuvuruga. Basi ni wangapi wangejisikia lingekuwa ni jambo zuri sana, mnaona, ku—kusanyiko ambalo sisi . . .

¹⁹ Kanisa hili ni kama letu huko juu, kanisa linalojitawala. Tunajisikia ya kwamba watu walio wengi wangukuwa na usemi kuliko mtu mmoja tu, mnaona, kwa kuwa hilo ndilo wanaloliita “kupiga kura.” Je, mngifikiri ingekuwa ni vema kuwa na ibada ya u—u—utambuzi usiku wa leo? Inua mkono wako kama unajisikia ya kwamba hilo lingekuwa ndilo jambo la kufanya. Vema. Hebu tuone. Sasa kinyume, ingekuwa tu . . . Vema. Tutawasambazia watu kadi za maombi basi, usiku wa leo, na kuwaita watu. Huenda kukawa . . . Endapo kuna wengi sana wao, nitamtuma Gene ama Billy, ama mmoja wao, huku chini alasiri ya leo. Yapata . . . Mnaanza ibada yenu saa ngapi, Junie? [Ndugu Raymond Jackson anasema, “Saa moja u nusu.”—Mh.] Saa moja u nusu. Saa kumi na mbili u nusu, basi, nao watawapa kadi za maombi. Nasi tutamwomba kila mtu aliye na hizo kadi. Hiyo inamaanisha kila mtu ataweza kuombewa, bali tutaninii . . . katika kusanyiko dogo. Ila kile tutakachofanya, tutaliacha lizunguke mstarini. Hebu . . . Nitawaambia wawape kadi za maombi wageni, kisha watu wa nyumbani wafuate, maana itakuwa ni watu wa nyumbani walio karibu, mnaona, kwa hiyo wataninii . . . Wanaelewa.

²⁰ Sasa, wakati mwingine, nyumbani hapa, kidogo ni vigumu kuwa na mkutano wa utambuzi. Bibi Wood ameketi karibu sasa. Nilishuka kwenda kanisani, nami ngingekuwa na ibada ya . . . Ningesema, “Sasa . . .” Nasi huenda tukalifanya hivyo usiku wa leo. Kabla hapajakuwapo na kadi zozote za maombi ama chochote kilichosambazwa, Roho Mtakatifu angekuwa karibu na kuwaita watu fulani. Nami ningesema, “Kila mtu hapa, aliye mgeni, simama.” Mnaona? Niache wote wasimame.

²¹ Ungesema, “Vema, huyu ni *nanii* kutoka,” lolote ambalo Roho Mtakatifu angesema, na kufanya hivyo.

²² Halafu wakati huo mwingine, ningegeuka na watu wengi sana hapa katika mji wetu huu, wangesema, “Vema, sisi hatukuwajua watu hao. Hatukujua walikuwa na shida gani. Huenda huo ulikuwa ni uongo.”

²³ Wakati mwingine, tuseme, “Vema, tutawachukua tu jamaa walioko nyumbani, hebu wasimame.”

²⁴ “Mbona, yeye aliwajua hao watu. Hakika, aliwajua.” Kwa hiyo, mnaona, Shetani ana mtego uliotegwa, kila mahali, mnaona. Yu—yuko tayari, wakati wowote.

²⁵ Na kwa hiyo baadhi yao wanasema, “Vema, kama una utambuzi huo tu wa moja kwa moja namna hiyo, hao watu wengine hawapati nafasi ya kuingia mstarini.” Wengine wao wanasema, “Vema, kama unayo, afadhali niombewe.” Vema, vema, ni vinginevyo tu. Kwa hiyo tuna, kwanza, njia moja, kisha

nyingine. Na, wao, watakuwa hivyo mpaka Yesu atakapokuja. Unaweza . . .

²⁶ Injili sikuzote huleta umati uliochanganyika. Matokeo ya kuhubiriwa kwa Kristo sikuzote husababisha umati uliochanganyika. Huwaleta tu waaminio, wanaojifanya waaminio, na wasioamini. Hilo ndilo kusanyiko ulilo nalo. Kwa hiyo tunatarajia yote hayo. Kwa hiyo tunatazamia mpaka . . . usiku wa leo ukiwa ni wakati mkuu katika Bwana. Sasa, kabla tu hatujalifungua Neno . . .

²⁷ Nanyi mnawaachilia yapata saa tano u nusu, nadhani, Ndugu Junior? [Ndugu Jackson anasema, “Chukua muda mrefu utakao, Ndugu Branham.”—Mh.]

²⁸ Halafu basi hao watu wanaotaka kuwa kwenye mstari wa maombi, usiku wa leo, basi wanaweza kuwaweka mstarini, kama likija kundi kutoka nje, basi tunaweza kuwaingiza ndani, mwajua, kupita milangoni, na kadhalika. Njoni saa kumi na mbili u nusu.

Na tuviinamishe vichwa vyetu sasa kabla hatujalisoma Neno.

²⁹ Bwana wetu wa thamani, tunakushukuru Wewe, kwa unyenyekevu sana, kutoka kwenye vilindi vya moyo wetu, kwa ajili ya tumaini hili lililo hai tulilo nalo ndani ya mwili huu unaokufa, kwamba kuna Bwana Mungu, na Yesu Kristo, na kupitia rehema Yake, na wema Wake, Yeye ametupatia Uzima wa Milele. Na tumaini hilo kuu liko ndani yetu leo hii, nasi tunalisikia kama ki—ki—kisima kinachobubujika nafsini mwetu, kikitupatia hakikisho kwamba Maneno yote ya Mungu ni ya kweli. Basi tuna furaha sana kujua, leo hii, ya kwamba haitupasi kubahatisha tu juu yake. Si kubahatisha tena. Ni kujua kweli. Kwa maana tumesoma ahadi Yake na kumwona Yeye akija na kuitimiza ahadi hiyo kwa Neno. Kwa hiyo, tunajua ya kwamba ni kweli. Nasi tunashukuru kwa ajili ya Roho Mtakatifu, Ambaye ni shahidi wa kufufuka Kwake.

³⁰ Nasi tunashukuru kwa ajili ya wahudumu, manabii wa kweli wa Mungu, wanaoitetea ile Kweli, na kuitetea haki. Basi tunaomba ya kwamba utawabariki watu hao leo hii, popote walipo, mimbarani mwao kote ulimwenguni, kwamba Roho Mtakatifu atatenda kazi juu yao, katika nguvu. Na kuwapa Neno Lako, na jalia litoe matokeo makubwa kila mahali, kwa kuwa tunaamini ya kwamba Kuja kwa Yesu kumekaribia.

³¹ Tungekuomba ulibariki kanisa hili dogo, leo hii, mchungaji wake, na mashemasi, na halmashauri yote, na washiriki, na wageni waliokusanyika malangoni petu. Tunashukuru kwa ajili ya ushirika; kumsikia mtu fulani akisema waliendesha gari maili nyingi, kuja kwa ajili ya ibada. Na kweli Maandiko yamedhihirishwa, wakati yaliposema, “Nikiinuliwa juu, nitawavuta watu wote Kwangu.”

³² Nasi tunajua, Bwana, ya kwamba Kanisa Lako haliko kwenye wingi, asubuhi ya leo. Waaminio wa kweli wako kwenye uchache. Lakini siku moja, Bwana, Wewe utawachukua hao wachache Kwako. Hiyo ndiyo saa tunayotamani. Hiyo ndiyo siku tunayongojea ipambazuke, hapo tutakapomwona, Yeye “aliyejeruhiwa kwa makosa yetu, na akachubuliwa kwa maovu yetu, na adhabu ya amani yetu juu Yake, na kwa kupigwa Kwake sisi tuliponywa.” Jinsi tunavyokushukuru Wewe kwa ajili ya jambo hili!

³³ Tunaomba, Bwana, ya kwamba Wewe utambariki mtumishi Wako asiyestahili, ninapojaribu kuwahudumia watu Wako. Wape kitu fulani ambacho kingetuleta sisi sote karibu na Wewe. Jalia tuondoke kwenye jengo hili, asubuhi ya leo, Mkristo bora kuliko tulivyokuwa tulipoingia. Pia jalia, akiwapo mmoja hapa asiye sawa, Bwana, wajalie waondoke humu jengoni asubuhi ya leo, wakiwa na moyo wenye furaha, wakishangilia kwa sababu wamepata Lulu ile ya thamani kuu, ambayo ilishinda mambo mengine yote ya maisha yao.

³⁴ Tungeomba, pia, Bwana, kwa ajili ya wale walio wagonjwa na wanaoteseka. Jalia isiwabidi kungojea ibada maalum usiku wa leo, lakini jalia Roho Mtakatifu mkuu amguse mtu huyo asubuhi ya leo. Wape neema Yako.

³⁵ Tumejaliwa, nikimwangalia mwanamke mmoja siku chache zilizopita, aliyekutana nasi, na kusema, “Loo, Ndugu Branham, inaonekana kana kwamba ugonjwa mbaya sana, uliolaani wakati mmoja katika Jina la Bwana, unajaribu kurudi tena. Lakini ninatulia kwa uchaji juu ya BWANA ASEMA HIVI.” Ndipo wakati madaktari walipomchunguza Dada yetu Bruce, walikuta “hana.”

³⁶ Tunashukuru, Bwana, ya kwamba Wewe hulitimiza Neno Lako. Ahadi Yako ni ya kweli! Jalia iwe ni BWANA ASEMA HIVI, asubuhi ya leo, kwa kila haja tunayohitaji.

³⁷ Tungewakumbuka wale walio hospitalini, na nyumbani, na hasa sana Ndugu yetu Rogers. Jalia neema na rehema Yako, kama imekupendeza Wewe, Bwana, nena asubuhi ya leo katika ono na utuonyeshe cha kumwambia ndugu yetu.

³⁸ Sisi ni watu Wako, tuingojea kulisikia Neno Lako. Mpaka tutakaposikia, tutakuwa tukitumainia kila dakika. Mwaga baraka Zako juu ya wote. Bariki kusomwa kwa Neno. Nasi tutakupa sifa zote na utukufu wote, kwa kuwa tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

³⁹ Ningependa nyote mfungue mlango wa 21 wa Mathayo Mtakatifu, tafadhalini. Nasi tutasoma sehemu ya Neno, kuanzia kwenye kifungu cha kwanza.

Hata walipokaribia Yerusalemu, na wakafika Bethfage, katika mlima wa Mizeituni, ndipo Yesu alipowatuma wanafunzi wawili,

Akawaambia, Enendeni katika kijiji kile kinachowakabili na mara mtaona punda amefungwa, na mwana-punda pamoja naye: wafungueni mniletee.

Na kama mtu akiwaambia neno, semeni, Bwana anawahitaji; na mara huyo atawapeleka.

Haya yote yamekuwa ili litimie neno lililonenwa na nabii, akisema,

Mwambieni binti Sayuni, Tazama, Mfalme wako anakuja kwako, mnyenyekevu, . . . amepanda punda, na mwana-punda, mtoto wa punda.

Wale wanafunzi wakaenda zao, wakafanya kama Yesu alivyowaamuru,

Wakamleta yule punda na mwana-punda, wakaweka nguo zao juu yao, . . . akaketi juu yake, hapo juu.

Watu wengi katika ule mkutano wakatandaza nguo zao njiani; na wengine wakakata matawi ya miti, wakayatandaza njiani.

Hata mkutano waliotangulia, na wale waliofuata, wakapaza sauti, wakisema, Hosana, Mwana wa Daudi: Ndiye mbarikiwa ajaye kwa jina la Bwana; Hosana juu mbinguni.

Hata alipoingia Yerusalemu, mji wote ukataharuki, watu wakisema, Ni nani huyu?

Makutano wakasema, Huyu ni yule nabii, Yesu, wa Naz- . . . ya Galilaya.

⁴⁰ Ninataka kusoma, ama kuchukua kama somo asubuhi ya leo, hayo maneno matatu ya mwisho ya kifungu cha 10: *Ni Nani Huyu?* Bwana na aongeze baraka Zake kwenye kusomwa kwa Neno Lake.

⁴¹ Hapana shaka ilikuwa yapata, tuseme, yapata saa nne Ijumaa asubuhi. Nao watu walikuwa wameamka tangu mapambazuko, wakitembea mjini. Ulikuwa umejaa sana, wakati huo, kufikia . . . Walikuwa wakilala nje ya kuta za huo mji, sakafuni, katika mahema yao, popote wangepata mahali pa kulala chini. Kwa sababu, wakati huu maalum ulikuwa umewavuta watu pamoja kutoka kote katika ulimwengu uliojulikana.

⁴² Iliitwa sikukuu ya pasaka, ambayo ilikuwa imewekwa na Mungu, kwa Wayahudi, huko nyuma kabisa kwenye nyakati za mwanzoni za historia yao. Ilikuwa ni ambapo mwana-kondoo wa sadaka alikuwa auawe, nao upatanisho ufanywe kwa ajili ya dhambi za hao watu.

⁴³ Nayo hii, ikiwa ni ya kila mwaka, kila mwaka ilitendeka. Lakini wakati huu ulikuwa ni wakati maalum. Kulikuwako na jambo fulani tofauti kidogo lilikuwa linaenda kutukia kuihusu

hii, mwajua. Na, kwa kawaida, mahali tunapofanyia ibada, tunapofanyia ibada yetu ya kawaida na ninii yetu... na ibada yetu, na kutoa zaka zetu, na kukusanyika makanisani mwetu na kushiriki pamoja na watu wetu. Bali, mnajua, Yesu anapokuja, siku zote ni kitu maalum. Kuna kitu fulani tu tunachoweza ku sema. Kulikuwako na matarajio makubwa. Hewa ilionekana kujawa na kitu fulani.

⁴⁴ Na hilo karibu lingenda sambamba na wakati huu sasa. Hewa imejaa leo hii matarajio ya Kuja Kwake mara ya pili.

⁴⁵ Kuna wengi mjini wakati huo, ambao hawakujua kitu juu yake, kama tu ilivyo ulimwenguni leo hii. Pia kulikuwako na wengi, kama walisikia, wasingekali hata kidogo kulihusu. Na hivyo ndivyo ilivyo ulimwenguni leo hii, kwa kuwa mambo mengine yanavutia sana kuliko ninii... kwa wanaume na wanawake wa ulimwenguni, kuliko kikomo cha Milele cha nafsi yao.

⁴⁶ Ila kulikuwako na wengine waliomwamini. Walikuwa wakimtarajia kuja, huku wakijua ya kwamba jambo fulani maalum lingekuwako. Jambo fulani lilikuwa linaenda kutukia. Kwa kuwa Yesu hawezi kuja, katika wakati wowote, isipokuwa jambo fulani maalum litendeke. Sikuzote jambo fulani jipya, wakati Yeye anapoonekana. Nao walikuwa wamejaa matumaini.

⁴⁷ Lakini jambo baya kuhusu haya yote, kulikuwa na wengi ambao hawakumwona, kamwe hawakuweza kumwona hapo alipokuja. Basi hilo ndilo moja ya mambo ya huzuni kuhusu siku hizi. Kutakuwako na wengi ambao hawatamwona hapo atakapokuja.

⁴⁸ Bali kutakuwako na masalia. Kutakuwako na wale wanaomjua Mungu, na ambao wanangojea, na walio na matarajio makubwa. Watamwona. Kwa kuwa atakuja kama mwizi usiku. Tutanyakuliwa kumlaki Bwana hewani, kule kuondoka kisiri kwa Kanisa.

⁴⁹ Loo, nawaambia, nikijua haya yote, awali, kwa Neno la Bwana, inatupasa kuomba na kusoma kila saa ya maisha yetu, tukijiandaa kwa ajili ya tukio hilo kuu. Na wakati hewa imejaa Uwepo Wake, na wakati tukiamini, na wahudumu waliotiwa mafuta wa Injili wakituma radi za maonyo, inatupasa kuwa tayari, dakika yoyote, kwa ajili ya tukio hilo lililobarikiwa, wakati tutakapowaona wote waliokufa katika Kristo, kote katika nyakati. Wakati tutakapomwona Yesu akija kulichukua Kanisa Lake, ndipo tutanyakuliwa kumlaki Yeye hewani.

⁵⁰ Kulikuwa na wengi ambao hawakumwona Yeye siku hiyo. Na wakati walipokuwa walingojea, nadhani, tangu mapambazuko, makusanyiko madogo yalikusanyika mahali mahali kote mjini, nao walikuwa wanajadiliana, wakisema, "Nashangaa kama atakuwa hapa kwenye Pasaka."

⁵¹ Ninaweza kumsikia maskini mhudumu mkweli akisimama na kusema, “Naam, kusanyiko, tunaweza kumtarajia, kwa sababu Yeye ni Mwana-Kondoo.” Mtu fulani aliyevuviwa na Roho Mtakatifu, aliyemjua Mungu na aliyajua Maandiko, na kujua kutimizwa kwa Neno Lake kulikuwa kumekaribia. “Atakuwa hapa, pasipo tashwishi hata kidogo, kwa kuwa Yeye ndiye Mwana-Kondoo wa Pasaka.”

⁵² Basi mnaweza kuwazia wakati kusanyiko hili lilipokusanyika pamoja na lile kusanyiko dogo kwenye lango, na baada ya muda kidogo wakasema, “Huenda akaja kupitia lango *hili*, ama huenda akaja kupitia lango *lile*.” Bali haikuleta tofauti yoyote Yeye angepitia lango gani. Walikuwa wamwone, haidhuru, kwa sababu ilikuwa ni ahadi.

⁵³ Kama anakuja leo hii katika wingu, ama juu ya farasi, haileti tofauti yoyote kwangu jinsi anavyokuja. Tutamwona, kwa vyovyote vile, kwa maana ni ahadi aliyotoa Mungu.

⁵⁴ Nao walikuwa wakingojea kwa matumaini makuu. Sherehe zilikuwa karibu kuanza hekaluni. Maji tayari yalikuwa yakimwagika kutoka mwambani, ambapo kusanyiko lilikuwa likiingia kuabudu. Makuhani walikuwa wamevaa mavazi yao marefu na ninii za—zao...majoho yao yote ya sherehe. Kila kusanyiko lilikuwa limekusanyika katika mahali pao palipofaa, Mafarisayo katika kona yao na Masadukayo katika kona yao.

⁵⁵ Kama hiyo si picha ya leo hii, siujui. Wamethodisti katika kona moja, Wabaptisti katika kona nyingine, Wapresbiteri katika kona nyingine. Lakini, mahali fulani, huku wametawanyika miongoni mwao, katika makundi madogo, liko Kanisa la Mungu aliye hai, lisilojali sherehe, bali wakikungojea kuonekana Kwake, wakiungojea wakati huo uliobarikiwa. Wakati hao wengine wanavutiwa tu na sherehe, sikukuu ya vibanda na taratibu za dini, bali Roho wa Mungu ameibadilisha mioyo yetu, hata tunajua Yeye yuaja karibuni.

⁵⁶ Basi walipokuwa wakingojea, mara, kutoka juu ya kilima likaja kusanyiko dogo likishuka chini, Mtu ameketi juu ya maskini nyumbu mweupe, akija polepole kuelekea langoni. Watu wakaanza kupiga mayowe, wakivunja matawi ya miti, na kutandaza nguo zao njiani, wakipiga makelele, “Hosana Kwake ajaye katika Jina la Bwana!”

⁵⁷ Ndipo maskini yule nyumbu akaendelea mbele, akiyatimiza Maandiko ya nabii, kasema, “Ee binti Sayuni!” Mnaona ilikuwa ni nini? Ilikuwa ni Kanisa, Wateule. “Bwana wako yuaja kwako, mnyenyekevu na mpole, ameketi juu ya maskini nyumbu, akimwendesha.”

⁵⁸ Na leo hii, wakati kanisa likingojea, moja ya siku hizi, akishuka kutoka angani, Yeye atakuja amepanda farasi mweupe. Mnaona kwamba nyeupe sikuzote imewakilishwa? Maskini, nyumbu mweupe, Yeye alikuja, ilikuwa ni kutanguliza

kuja, amepanda farasi mkubwa wa vita, huku mavazi Yake yamechovywa katika Damu, Jina juu Yake lililoitwa, “Neno la Mungu.” Huko ni kuja Kwake sasa. Yale makundi madogo yamekusanyika, yanaangalia, yakingojea kuonekana kule. Basi itakuwa ni furaha jinsi gani tutakapoendelea mbele, tukiyavunja matawi, tukipaza sauti, “Hosana Kwake ajaye katika Jina la Bwana.”

⁵⁹ Ilisababisha taharuki kubwa sana miongoni mwa watu, Wamethodisti na Wabaptisti wa siku hiyo, Mafarisayo na Masadukayo, na watu mbalimbali, mpaka wakasema, “Ni nani Huyu ajaye? Vurugu hii yote inahusu nini? Hatuoni tishio lolote kulihusu. Yule ni Mwanadamu tu, Naye amempanda maskini nyumbu. Hakuna chochote cha kuhofia. Kwa nini vurugu hii yote na makelele chungu nzima? Ni Nani?”

⁶⁰ Kabla tu ya kule Kuja kwa Bwana Yesu, Yeye alimtuma Roho Mtakatifu kwa Kanisa, katika siku hii ya mwisho. Naye Roho Mtakatifu amekuwa ni shahidi wa kufufuka Kwake, na amethibitisha ya kwamba Yeye yu hai. Naye yuaja. Nalo Kanisa linajitayarisha. Basi tunapoliona kanisa likijitayarisha, likiachana na uasherati, likiachana na ibada za sanamu, likiachana na tamaa mbaya na kazi zote za mwili. Sisi, Kanisa na watu, tunayaona hayo makusanyiko madogo yakikusanyika, wakiacha unywaji wao pombe, wakiacha udanganyifu wao, wakiacha umbeya wao, wakiacha kila kitu kilicho cha kimwili, wakijifanya tayari, wakipiga makelele kwa sauti zao zote, na kupiga makofi na kupiga makelele ya ushindi.

⁶¹ Watu wanasema kwa sauti kuu, “Ni Nani Huyu?” Hawaelewi. Hawakuelewa wakati huo; Yeye alikuja, mnyenyekevu na mpole, alikuja amepanda nyumbu. Naye amekuja, leo hii, kwa maskini na wanaoteseka. Ambapo, hao wengine wanasema, “Hakuna kitu kama uponyaji. Hakuna kitu kama ubatizo wa Roho Mtakatifu. Wote ni lundo la upuuzi. Hakuna kitu kwake.”

⁶² Lakini ni vivyo hivyo tu, Yeye amekuja, akithibitisha kufufuka Kwake. Kila ishara aliyofanya duniani, Yeye anaifanya sasa hivi katika umbo la Roho Mtakatifu. Kuna matarajio miongoni mwa watu. Wanangojea lile tukio kuu la kukaribia Kwake hivi karibuni. Tunajua haitachukua muda mrefu hata tutakapomwona Yeye Ambaye tumempenda. Nasi tunaamini ya kwamba haitachukua muda mrefu sana mpaka mambo yote yaliyotabiriwa katika Maandiko yatakapotimia.

⁶³ Sasa, kwenye kusanyiko hilo siku hiyo, kulikuwa na maoni yaliyotofautiana. Baadhi yao walilia, “Kwani ni Nani? Ni kitu gani kinachosababisha vurugu hii yote? Kwa nini kundi hilo la Wagalilaya, watakatifu wanaojibingirisha, linapiga mayowe na makelele namna hiyo?”

64 Ninaweza kumwona maskini mwanafunzi mmoja mwema akipanda pale na kusema, “Hivi hamjui, ndugu zangu? Huyu ni yule Nabii wa Galilaya. Huyu ni Yesu wa Nazareti, aliyenenwa habari zake na Maandiko. Hivi hamjui Maandiko yanasema, ‘Yeye atakuja, amepanda juu ya mwanapunda?’ Naye atakuja kwa watu Wake. Na hiyo ndiyo sababu hao wanapiga makelele jinsi wanavyofanya. Tumekuwa kwenye mikutano ya Mtu huyu. Tumemwona akiwafufua wafu. Tumemwona akiyafungua macho ya vipofu. Tumemwona akisimama pale na kuangalia nje kwenye kusanyiko Lake, na, ‘Mbona mnawazia moyoni mwenu?’ Tumemwona akifanya ishara kuu, nasi tunajua huyo ndiye Masihi.”

65 Walikuwa umati uliochanganyikana. Baadhi yao wakasema, “Vema, huenda ikawa kwamba Yeye *anaweza* kuwa ni kitu kama hicho.”

66 Sasa, hivyo si ni vile tu wanavyojisikia siku hizi? “Haya yote yanahusu nini? Kuna kitu kama Roho Mtakatifu? Ni kitu gani kinachowafanya hao watu watende jinsi wanavyotenda?”

67 Mbona, ni kionjo cha awali cha utukufu wa kiungu. Ni Nguvu fulani. Ni Roho Mtakatifu aliye hapa duniani, akimwakilisha Kristo, kivuli tu cha Kuja Kwake. Mambo haya yote yalitabiriwa yangetukia kabla tu Yeye hajaja tena. Nasi tunajua hilo. Hiyo ndiyo sababu tumesisimkwa nalo. Hiyo ndiyo sababu tuna shauku yake.

68 Inaleta tofatuti yoyote yale watu wengine wanayosema, hilo halijalishi hata kidogo. Watu wanasema, siku hizi, “Huyo ni nani?”

69 Siku zile, wao walisema, “Hatujui Yeye ni nani, Yesu wa Nazareti. Vema, tutaenda kule na kuangalia kwenye zile amri, nasi tutaona kama Yeye alikuwa ni mfuasi wa dhehebu *hili*. Tutaona kama Yeye alikuwa ama ni Mfarisayo au Msadukayo, au Mherodia, ama chochote awezacho kuwa. Tutaangalia.” Nao wasingeweza kupata kumbukumbu yoyote ya masomo Yake, juu ya digrii yoyote aliyokuwa nayo. Ndipo basi wakarudi tena, “Ni nani Yeye? Yeye si mfuasi wa yoyote ya mapokeo yetu. Hajaunganika na yoyote na ninii zetu. . . Hajashirikishwa na lolote la mashirika yetu. Hana digrii zozote. Hatuna kumbukumbu Yake yoyote kwenda shuleni. Kamwe hakuwa katika seminari. Wala haijadaaiwa kwenye—kwenye. . . kwenye vitabu *hivi* ama vitabu *vile*. Hatumwoni popote. Ni nani Yeye?”

70 Vitambulisho vyake vyenyewe vilikuwa ni zile kazi ambazo Mungu alimpa kufanya. Yeye alisema, “Nisipozitenda kazi za Mungu, basi msiniamini Mimi.”

71 Walikuwa na njia yao wenyewe ya kuamini, kwa vitambulisho vya mtu, kwa dhehebu alilokuwa mfuasi wake. Ni kama tu vile ilivyo siku hizi, yeye anajulikana kwa vitambulisho vyake vva kimadhehebu.

⁷² Bali mtu wa Mungu, Roho Mtakatifu aliye miongoni mwa watu, anakuja juu ya watu, anakuja juu ya mhudumu, anakuja juu ya kusanyiko, na kujitambulisha kwamba Huyu ni nani; sio kwa dhehebu, bali kwa Nguvu za kufufuka kwake Yesu Kristo, kutanguliza Kuja Kwake. Loo, ni saa ya jinsi gani tunayoishi! Mitende mikononi, nguo mgongoni, tayari kuzitandaza njiani, “Heri Yeye ajaye katika Jina la Bwana!” Ni kitu gani kilichokuja katika Jina la Bwana? Roho Mtakatifu. Yeye ajapo, atawaonyesha mambo yajayo. “Hatanena kwa shauri lake Mwenyewe, bali atanena habari Zangu,” kasema Yesu. Basi Roho Mtakatifu huja kufanya kazi Yake katika Jina la Bwana Yesu. Kote kutoka mimbarani hadi kwenye kidimbwi cha kubatizia, hadi kwenye ibada ya uponyaji, hata mahali pengine pote, “katika Jina la Yesu Kristo,” akikuangalia kule Kuja kwa Bwana, akilitayarisha Kanisa kama mtangulizi. Kama vile Yohana Mbatizaji alivyokutangulia kule kuja mara ya kwanza, Roho Mtakatifu yuko kanisani, akikutangulia, akilifanya Kanisa tayari kwa ajili ya Kuja mara ya pili.

⁷³ Nao ulimwengu unalia kwa sauti kuu, “Ni nani huyu? Walitoka wapi? Wana vitambulisho gani? Wametoka kwenye shule zipi?” Huwapati kwenye kumbukumbu. Liko Utukufuni, mahali walipotoka. Mbinguni ndiko ziliko kumbukumbu zao. Kwa kuwa Ufalme wao sio wa ulimwengu huu, bali ni wa ulimwengu ujao. Shauku yao si ya ulimwengu huu. Ni ya ulimwengu ujao; mitindo yao, shauku zao. Hiyo ndiyo sababu yale mavazi, na matendo, na tabia za watu wa ulimwengu ni kinyume sana.

⁷⁴ Kwa kawaida utatenda, wewe, kwa kawaida utatenda kama roho aliye ndani yako. Anayachochea maisha yako. Anakufanya kile ulicho, ni uhai ulioko ndani yako. Na wakati wanaume na wanawake wanapodai kwamba ni Wakristo, na wangali wanataka kuwa kama ulimwengu, kuna kasoro mahali fulani, kwa kuwa sisi si wa ulimwengu huu. Kwa kuwa roho yetu, kama tungalikuwa Wajerumani, tungeupenda Ujerumani. Kama tulikuwa Ufini, tungetenda kama watendavyo huko Ufini. Kama wao ni Wamarekani, wana roho ya Marekani. Iwapo sisi ni Wakristo, tunayo Roho ya Kimbinguni. Nazo roho zetu zinatoka huko Juu. Hizo huyaelekeza maisha yetu na mawazo yetu. Huo ni upendo wa kitauwa, wa kindugu; maisha safi; watu wenye heshima, wanaoheshimika.

⁷⁵ Sasa, mle ndani, walisema wengine walikuwa wakimuunga mkono, wengine walikuwa wakimpinga.

⁷⁶ Sasa, kunao watu siku hizi ambao wanapinga kwa dhati kitu chochote kinachoitwa Mungu; hawana dini. Nao zaidi sana ndio wengi, nchini mwetu. Ulimwenguni kote, hao ndio wengi, mamilioni na mamilioni ambao hawajawahi kusikia Jina la Yesu Kristo. Wao ndio wengi.

⁷⁷ Halafu kunao wale ambao wanakiri dini. Nao wanapenda kuendeleza sherehe zao. Wanapenda kuwa watu mashuhuri. Wanapenda kuvalia, na kwenda kanisani na kuwa na namna fulani za nyimbo za dini, na u—ujumbe mdogo wa namna fulani, wanazungumza juu ya Mungu aliyekuwako, kisha wanamweka huko nyuma kabisa katika historia, hata hawezi kutenda kazi, kwamba Yeye ni kitu kilichokuwako. Wanataka kudai, kwamba, “Yesu ni wa kweli. Yeye alikuwa ni jamaa mzuri. Alikuwa Mtu mashuhuri. Alikuwa kama Washington, kamwe hakusema uongo; ama kama Napoleon.” Huo ndio msimamo wao kumhusu Yesu. Wanafikiri ya kwamba alikuwa ni mtu mzuri tu. Wengi wao siku hizi hawadai kwamba Yeye alikuwa ni wa Kiungu. Wao wanadai tu kwamba Yeye alikuwa ni mtu mwema, ya kwamba mafundisho Yake yalikuwa sahihi. Baadhi yao wanamwamini Yeye kuwa ni nabii tu.

⁷⁸ Lakini kuna wale wanaovuka mpaka huo. Ninamwamini Yeye kuwa ni Mungu, “Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele,” kwamba Yeye hakuwa tu ni nabii, ya kwamba Yeye hakuwa tu mwanadamu, ya kwamba Yeye hakuwa tu ni mwalimu, au mtu mwema. Yeye alikuwa ni Yehova Mungu wa Kiungu akiishi katika mwili wa nyama. Ungeniuliza, “Ni nani Huyu?” Hayo ndiyo maoni yangu kumhusu. Yeye ni Mungu, aliyedhihirishwa katika mwili, kuondoa dhambi za ulimwengu. “Ni nani Huyu?” Sio tu mwanadamu, sio tu nabii, bali ni Imanueli, Mungu pamoja nasi. Halafu, sio tu pamoja nasi, bali ndani yetu, kupitia kwetu, Mungu katikati yetu.

⁷⁹ Basi, kama hiyo ni kweli, Mungu wa kimbinguni hawezi kubadilisha asili Yake iendane na asili ya watu. Watu hawana budi kubadilisha asili yao iendane na mipango ya kimbinguni ya Mungu. Hiyo ndiyo sababu watu wanalia, “Ni nani Huyu?” Ni Mungu katikati ya watu Wake. Hawalielewi. Mungu kamwe hatakuja kwenye kiwango chako. Itakubidi kuja kwenye Chake. Mungu hatakuja kwenye matakwa yako. Inakubidi kuja kwa ya Mungu. Ndipo basi wakati matakwa hayo yametimizwa, juu ya ahadi ambayo Mungu alifanya, kuwakomboa watu. Kama matakwa hayo yametimizwa, utu wako wote unabadilika. Mawazo yako yanabadilika. Tabia zako zinabadilika. Kila kitu kukuhusu wewe kinabadilika. Shauku zako zinabadilika. Maisha yako yanabadilika. Tabia zako zinabadilika. Unabadilika. Kila kitu kukuhusu wewe kinabadilika, maana kuna Maisha mapya ndani yako.

⁸⁰ Hilo ndilo linalowafanya watu siku hizi kusema, “Ni nani Huyu? Huyu ni jamaa yule aliyekuwa akifanya kazi huku? Huyu ndiye huyo? Ni nani huyu?” “Alienda shule wapi? Ana vitambulisho gani?” wanasema wahubiri. Wapi... “Ni nani mwanamke huyu? Huyu siye yule mwanamke niliyekuwa nikimwona huko nje mtaani?” Naam. “Ana shida gani?” Jambo fulani lilitukia. “Huyu siye yule mwanamke aliyekuwa akivaa

kaptura?” Lakini jambo fulani lilitukia. “Huyu si ndiye yule mwanamume aliyekuwa akivuta sigara?” Lakini jambo fulani lilitukia. “Huyu si ndiye yule mtu aliyekuwa akinywa pombe?” Lakini jambo fulani lilitukia. “Huyu si ndiye yule mwanamume na mwanamke waliokuwa wakilaani na kwenda kwenye vilabu vya usiku?” Lakini hawafanyi hivyo tena. “Ni nani huyu?” Ni Roho Mtakatifu, ule Utu wa Mungu, akiishi ndani yao. “Nitashuka niende makanisani mwao, nijue kuna nini.”

⁸¹ Kama vile Mafarisayo walivyofanya, walisema, “Tutaenda langoni. Tupate kujua wanalosema. Tutaona kwamba Jamaa huyu ni Nani, juu ya maskini nyumbu huyu mweupe, akimpanda kutelemka kilimani.”

⁸² Basi walipofika malangoni, watu hawa kweli walikuwa na wakati mzuri. Walipiga mayowe na kupiga makelele. Walipaza sauti na kumsifu Bwana.

⁸³ Nalo lilikuwa ni kinyume sana na dini yao ya siku hizo, hao makuhani na marabi waliosimama pande zote. Wakasema, “Wanyamazishe. Hatutaweza kusikia yale daktari atakayosema, ama yale, kasisi. Wanyamazishe.”

⁸⁴ Yesu, ninaweza kumwona wakati akigeuka, kasema, “Wakinyamaza, mawe mara moja yatapaza sauti.” Ilibidi jambo fulani litendeke.

⁸⁵ Kasema, “Mawe yangeweza kulia?” Mungu yeye yule aliyeyaumba alikuwa amepanda juu yao. Kwa nini wasingeweza kusema, “Wanyamazishe”? Wasingeweza kunyamaza.

⁸⁶ Hivyo ndivyo ilivyo siku hizi, wakati kusanyiko limekusanyika pamoja. Huko kutanguliza kuonekana Kwake, Roho Mtakatifu alianza kuwapulizia. Wanaona hizo ishara na maajabu yakifanywa na Roho Mtakatifu. Hawawezi kunyamaza. Kitu fulani kitapiga kelele.

⁸⁷ Nao ulimwengu wa kanisa ukasema, “Ni nani Huyu? Haya yote yanahusu nini? Kwani wewe ni mmoja wao? Ni kitu gani kilichosababisha haya yote?” Hawalipati. Wala hawalipati siku hizi. Hawakulipata wakati huo. Kamwe hawatalipata.

⁸⁸ Upako wa Roho Mtakatifu umelileta hilo kwa ulimwengu wa kanisa. Umelileta. Mnaona?

⁸⁹ Hayo hapo yale matabaka matatu. Asiyeamini, anayejifanya mwaminio, na mwaminio halisi. Na mara nyingi, wanaojifanya waaminio wanaingia miongoni mwa waaminio halisi, nao wanalia, bado, “Ni nani?”

⁹⁰ Ni nani Huyu atakayeingia kwenye kusanyiko, ambaye atalitia mafuta hata mmoja atanena kwa lugha, na mwingine atoe fasiri, amwambie mwenye dhambi kuhusu dhambi zake hasa na mahali alipo? Ni nani Huyu anayesimama, na mwanamke asiye na elimu ambaye hawezi kusoma jina lake, naye atasimama chini ya huo upako wa Roho Mtakatifu na

kunena maneno ambayo hajawahi kuyasikia? Kisha Mmekisiko anasimama kanisani na kusema, “Nilielewa kila neno lake. Na hata kuniita kwa jina langu, naye ameniita nikatubu. Basi Mungu na airehemu nafsi yangu.” Ni nani Huyu? Ni nani anayeweza kumchukua mkulima asiye na elimu, naye anaweza kusimama chini ya uvuvio, na kumwambia mtu kwamba yeye ni nani, na mahali anakotoka, na kile kilichompata, na yale anayopaswa kufanya, na kwamba matokeo yake yatakuwa nini.

⁹¹ Ulimwengu unalia, “Ni nani Huyu? Ni kitu gani Hiki? Kilitoka wapi?” Ni Roho Mtakatifu, alitoka kwa Mungu. “Kwa kusudi gani?” Kuwatayarisha watu, kuwapa mazingira ya Kimbinguni, shauku ya kupaa juu zaidi.

⁹² Sasa, si sana sana vile watu wengine wanavyofikiria, hilo. Jambo tunalowazia asubuhi ya leo, ni, “*Wewe* unafikiri ni nani?” Ni juu yangu na yako.

⁹³ Ni ushirika tu wa dhehebu linaloitwa Pentekoste, church of God, Pilgrim Hol- . . . ama Nazarayo, ama kitu kama hicho, church of God, Assemblies of God, kanisa la United Pentecostal? Hivyo ndivyo ilivyo? Kama hiyo ndiyo, wewe ni mwenye mashaka. Jambo ndilo hilo, dini yako ni dini tu. Haina wokovu ndani yake.

⁹⁴ Lakini kama ungalilichunguza, na kulipata, nafsi mwako, kuwa ni Yesu Kristo Mwana wa Mungu, basi, “Heri Yeye ajaye katika Jina la Roho Mtakatifu!” Hosana juu mbinguni, kwake Yeye ajaye katika Roho Mtakatifu, kwa sababu ni Roho wa Yesu Kristo Mwenyewe katika Kanisa Lake, akiwafanya wana na binti Zake, akiwapa asili Yake. Kwa kuwa mtaishi na Baba, pia, katika nyakati za Milele zijazo.

⁹⁵ “Ni Nani? Haya yote yanahusu nini?” Nako kule Kuja kwa Roho Mtakatifu daima kumeleta mambo kama hayo.

⁹⁶ Katika siku za Nuhu, wakati Roho Mtakatifu alipokuja juu ya Nuhu, naye akaanza kutabiri, na kuanza kusema kwamba unakuja wakati ambapo ulimwengu utaangamizwa kwa maji. Angalia jinsi lilivyokuwa kinyume na imani yao. “Kulikuwako na wenye kubeza na wenye kudhihaki,” ilisema Biblia, “wakifanya dhiihaka.” Walikuwa wakila, wakinywa, na kusherehekea, wakacheka machoni pa nabii huyo, na kushangaa, “Alikuwa ni nani?” Upesi walipata kujua alikuwa ni nani.

⁹⁷ Kila wakati Roho Mtakatifu anapokuja, Yeye husababisha utengano miongoni mwa watu. Anasababisha wakati ambapo mtu hana budi kusimama na kufanya uamuzi. Amekuja kwako. Amekuja kwangu. Hatuna budi kufanya maamuzi yetu.

Alikuwa katika siku za Nuhu.

⁹⁸ Pia alikuja katika wakati wa Musa, wakati Mungu alipomtia mafuta mtumishi Wake kwa Roho Mtakatifu, akamtuma huko

Misri. Wengine walisema, “Ni nani mtu huyu maalum? Ni nani jamaa huyu ambaye angejifanya mtawala juu yetu?” Musa hakutamani kuwa mtawala. Yeye alikuwa akiwaletea hao watu Ukweli. “Anafanya nini? Kuzivunja dini zetu.”

⁹⁹ Hivyo ndivyo walivyosema kumhusu Yesu. “Anazilaani dini zetu,” kwa sababu hizo ndizo tu walizokuwa nazo.

¹⁰⁰ Ndivyo ilivyokuwa katika siku za Nuhu, ama Musa. Musa alishuka chini na kuyararua mapokeo yao, na kuwaleta kwenye imani iliyo hai ya Mungu aliye hai, na kuwaongoza kutoka ushindi mmoja hadi mwingine, kwa ishara na maajabu. Iliwatatiza wasioamini. “Ni nani huyu? Mtu huyu ni nani? Alizaliwa wapi? Tulidhani alikuwa ni Mmisri. Hapa mara moja, hapana shaka ni mwana haramu mahali fulani. Ni nani anayekuja katika Jina hili?” Daima imekuwa hivyo.

¹⁰¹ Katika siku za Yesu, wao walisema, “Ni nani Yeye? Hana elimu. Hatuna shule, hatuna kumbukumbu ya masomo Yake. Hatuna dhehebu alilo mshirika wake. Ni nani Yeye? Jambo pekee tulilopata kujua, kulikuwako na mwendawazimu huku nje, mtu wa mwitu jina lake Yohana Mbatizaji, nywele zimetokeza kote usoni mwake, na nusu uchi, amejizungushia kipande cha ngozi ya kondoo, aliyekutangaza Kuja Kwake. Yeye... Naye alizaliwa mwana haramu. Mama yake alikuwa na mimba Yake, kabla Yusufu hajapata kumwoa mama Yake. Ni nani Huyu?” Hiyo ndiyo kumbukumbu Yake pekee waliyokuwa nayo. Jina la Bwana libarikiwe!

¹⁰² Hayo tu ndiyo wanayojua kulihusu Kanisa siku hizi, “Kundi la wachimba mashimo ya nguzo ama chochote kile,” hawana kumbukumbu hata kidogo. Hiyo Kumbukumbu haiwekwi kwenye vitabu vya duniani. Imelindwa kiungu Mbinguni. “Ni nani huyu? *Huyu* alikuwa ni mlevi. *Huyu* alikuwa ni *nanii*, *yule*.” Hiyo ni kweli. Lakini sasa yeye ni mwana wa Mungu, amebadilishwa.

¹⁰³ “Ni nani Yeye? Ni nani huyu ajaye katika Jina la Bwana?”

¹⁰⁴ Roho Mtakatifu anapokuja siku hizi, Yeye analeta uamuzi ule ule. Kila mmoja wetu anawajibika na uamuzi wetu. Hatuna budi kuufanya. Uko hapa karibu nasi. Uko hapa pamoja nasi. Hakuna njia ya kuuepuka tena. Hakuna kitu tunachoweza kufanya juu yake. Inatubidi kumkataa ama kumpokea. Uzima ule ule uliokuwamo katika Kristo Yesu uko Kanisani siku hizi. Unatenda kazi zile zile. Unafanya miujiza ile ile. Unafanya kila kitu Yeye alichofanya. Unawaponya wagonjwa, unawafufua wafu, unawataka wenye ukoma, unawatoa pepo, ukihubiri Injili. Maskini wanaupokea.

¹⁰⁵ “Heri yeye asiychukizwa. Nendeni mkamwonyeshe Yohana,” Yeye alisema, “mambo haya yanayofanywa.”

¹⁰⁶ Yohana, gerezani, macho yake ya tai yalikuwa yameingia utando. Jicho lake la kinabii halingeweza kuona kama lilivyoona

wakati mmoja. Lakini basi angeweza kuona, hapo aliposema, “Viwete wanatembea, vipofu wanaona, viziwi wanasikia. Na heri yeye asiye chukizwa na—na yale nifanyayo.”

¹⁰⁷ “Nisipozitenda kazi za Baba Yangu, basi msiniamini Mimi. Na kama nikizitenda kazi za Baba Yangu, iwapo hamwezi kuniamini Mimi, ziaminini hizo kazi.” Sasa, huo ulikuwa ndio ujumbe Wake. Hilo ndilo alilosema, kwamba halina budi kufanywa. Hivyo ndivyo inavyotubidi kufanya, ni kufanya uamuzi. Tutafanya nini nalo? Liko hapa. Ni nani? Ni kitu gani? Ni ahadi ya Mungu, kwa Neno Lake, ya kwamba Yeye angelitenda. Mungu aliahidi angefanya hivyo, nasi tunaona likifanywa. Sasa ni juu yetu kufanya uamuzi. Tutatumika? Tutaelewa?

¹⁰⁸ Unasema, “Nitawezaje, ndugu, kufahamu mambo nisiyojua kitu kuyahusu?”

¹⁰⁹ Yesu alimwambia Nikodemo, “Mtu asipozaliwa mara ya pili, hawezi kuona ama kuufahamu Ufalme wa Mbinguni.” Kasema, “Upepo huvuma upendako, upendako, wala huwezi kujua utokako, wala uendako; unapitia njia gani, ama uendako, ama umekuwa wapi. Ndivyo alivyo kila mtu aliyezaliwa na Roho.”

¹¹⁰ Hujui mahali anakotoka, mahali amekuwa, wala anakoenda. Bali unajua jambo moja, mahali atakapokupeleka. Popote atokapo, atakurudisha huko pamoja Naye. Kwa hiyo, siku hizi, inatupasa, kujua tunachofanya, kukielewa. Sasa, iwapo halishuhudii Neno, basi siye Roho wa Mungu. Kama hawaponyi wagonjwa, anaukana, basi siye Roho wa Mungu. Mungu ni mponyaji.

¹¹¹ Wakati mmoja, kama nilivyosema wakati mmoja, “Kwa nini Mungu kamwe akaiacha dhambi ije duniani?”

¹¹² Mungu alikuwa kitu kimoja wakati mmoja. Katika kitu hicho kimoja mlikuwamo na sifa. Naye alikuwa ni Mwokozi. Kimaumbile Yeye alikuwa ni Mwokozi. Kama kamwe hakukuwako na mwenye dhambi, Yeye angeweza kuwa Mwokozi? Asingeweza kuokoa mpaka alipoiruhusu dhambi.

¹¹³ Mungu ni mponyaji. Wala hawezi kuponya isipokuwa kuna mtu fulani aliye mgonjwa, apate kuponywa. Mnaona, kama kusingalikuwa na ugonjwa, kamwe kusingalikuwako na mponyaji. Mungu akiwa ni mponyaji, sifa Zake Mwenyewe ziliyaleta mambo haya. Ilibidi pawe na kitu Fulani cha kuitikia sifa hiyo iliyokuwa ndani ya Mungu.

¹¹⁴ Mungu, neno *Mungu*, linamaanisha “kitu cha kuabudiwa.” Mungu alitaka kuabudiwa, kwa hiyo ilimbidi kutoa kitu ambacho kingemwabudu Yeye. Yesu alimwambia yule mwanamke kisimani, “Mungu ni Roho, nao wamwabuduo imewapasa kumwabudu katika Roho na Kweli.”

¹¹⁵ Kwa hiyo Roho wa Mungu akiwa karibu, ni kitu gani kitakachotendeka? Wokovu utaletwa, wokovu utakaosababisha ibada ya kiroho. Sio kuimbwa kwa nyimbo, kwa jumla, bali ni ibada ya Roho. Haina budi kuwa kinyume sana na akili, inapumbazwa nayo. Huwezi kumfahamu Mungu kwa imani ya kiakili. Huna budi kuzaliwa mara ya pili. Haina budi kufika moyoni. Haina budi kuwa ni ujuzi. Ndipo wakati huo ujuzi unasababishwa na Roho Mtakatifu, basi asili ile ile na nguvu zile zile na tendo lile lile lililotukia kwenye Kanisa, mara ya kwanza, litakuja tena, kwa kuwa ni Mungu ndani yao.

¹¹⁶ Yesu alisema, “Bado kitambo kidogo na ulimwengu hautaniona tena, hata hivyo ninyi mtaniona, kwa kuwa Mimi...” “Mimi” ni kiwakilishi nafsi. “Nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata ukamilifu wa dahari. Ndipo kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya.” Ndipo wakati kazi hizo zinapotolewa Kanisani, zinawachochea watu, watu wa nje, kama ilivyofanya kule kwenye ile sikukuu.

¹¹⁷ “Ni nani Huyu? Hao watu wana shida gani?” Wakati hao Wagalilaya walipomwona akija amempanda maskini nyumbu huyo, walipiga mayowe na kupaza sauti, nao—nao wakaendelea kama ku—kundi la walevi. Hao makuhani, wangewafanya wanyamaze.

¹¹⁸ Akasema, “Wakinyamaza, haya mawe yatalia vivyo hivyo.” Mnaona?

¹¹⁹ Kwenye siku ya Pentekoste, wakati Roho Mtakatifu alipowajilia hao watu, walitenda kama walevi. Sana hata wakamdhihaki na kumfanyia mzaha, kasema, “Hawa watu wamejaa mvinyo mpya.”

¹²⁰ Petro akasema, “Ninyi watu wa Yerusalemu, nanyi mkaao Yudea, jambo hili na lijulikane kwenu, na myasikilize maneno yangu, kwa kuwa watu hawa hawajalewa kama mnavyodhani. Lakini hili ni lile lililonenwa na nabii Yoeli, ‘Itakuwa katika siku za mwisho, asema Bwana, nitaimwaga Roho Yangu juu ya wote wenye mwili.’”

¹²¹ Wakati Roho yuyo huyo anapomwagwa juu ya kusanyiko la watu, matokeo yale yale yatatukia. Kwa kuwa huwezi kutia uhai wa mzabibu katika mboga na kuufanya uzae maboga. Utazaa zabibu. “Kwa matunda yao wanajulikana.” Kanisa linajulikana. Ulimwengu unashangaa, “Ni Nani? Ni kitu gani hiki kinachoendelea?” Hawaelewi kwa sababu hawamjui Mungu.

¹²² Sasa, tunapooni hili likija kutimia, vile hasa Mungu alivyosema, tunangojea sasa. Ni kitu gani? Roho Mtakatifu anamtambulisha Kristo. Siku moja yenye utukufu, sio ng’ambo ya ubavu wa kilima, amepanda nyumbu, bali kutoka Utukufuni, atakuja Mwana wa Mungu, amevikwa haki ya Roho wa Mungu, amepanda farasi mweupe, huku vazi Lake limechovywa katika

Damu, anayeitwa “Mfalme wa mfalme, na Bwana wa mabwana.” Yeye atakuwa ni Neno la Mungu. Na wakimfuata kupitia angani, watakuwa ni elfu kumi mara elfu kumi wa maelfu. Majeshi ya Mbinguni yatakuja pamoja Naye. Huo utakuwa ni wakati wa utukufu jinsi gani! Kuimba, kutakuwako na kuimba. Kutakuwako na kupiga makelele.

¹²³ Kutakuwako na huzuni. Kutakuwako na kilio. Kutakuwako na kuomboleza. Kutakuwako na kulia.

¹²⁴ Wewe utawakilishwa katika moja ya makundi hayo, rafiki. Kwa hiyo fanya uamuzi wako asubuhi ya leo, utakuwa na kundi gani, tunapoviinamisha vichwa vyetu kwa dakika moja.

¹²⁵ Nashangaa kwenye wakati huu kama kuna yeyote ambaye hajafanya uamuzi wao, bado, kwa ajili ya Yesu Kristo. Hata hivyo, umekuwa kwenye hii mikutano, na kumwona akiwapa vipofu kuona, viziwi kusikia, viwete kutembea, ukimwona akiyachukua mawazo yenyewe ya nia za watu, na kusema, “Wewe ni *fulani-wa-fulani*. Kwa nini ukafanya *hivi* na kufanya *vile*?” Vile vile hasa Yeye alivyosema angefanya. Na, hata hivyo, bado hujawa mtumishi Wake. Kamwe hujapata shahidi.

“Hakuna mtu awezaye kumwita Yesu Kristo, ila kwa Roho Mtakatifu.”

Unasema, “Ninaliamini kwa sababu Neno linasema hivyo.” Hiyo ni kweli.

¹²⁶ Lakini Neno linasema, ya kwamba, “Hakuna mtu anayeweza kusema Yesu ni Kristo mpaka umempokea Roho Mtakatifu. Hakuna mtu anayeweza kumwita Yesu Kristo, ila tu kwa Roho Mtakatifu.”

¹²⁷ Hamjapokea hili bado? Nawe ungetaka, ungetaka kukumbukwa katika maombi kwa kuinua mkono wako, ukisema, “Niombeeni. Sasa ninakiri kwa Mungu ya kwamba ninamtaka Roho Mtakatifu maishani mwangu aniongoze, ili nifahamu kabisa mpango Wake wote alio nao kwa ajili yangu maishani, nipate kutembea pamoja Naye, kama mtumishi Wake.” Waweza kuinua mkono wako kabla tu hatujaomba? Bwana akubariki, mwanangu. Bwana akubariki, dada. Mungu awe pamoja nanyi.

Na tuombe.

¹²⁸ Mungu mwenye rehema sana, kama tulivyosoma katika Neno Lako kwamba wakati ulipoingia katika mji wa Yerusalemu, ambako watu Wako walikusanyika, kulikuwako na wale pale waliokuwa wakikutarajia Wewe. Hewa ilikuwa imejawa na Kuja Kwako. Ulikuwa umeahidi ya kwamba ungekuwa kwenye ile karamu, Wewe ungekutana nao mle, nao walikuwa wakikutazamia Wewe.

¹²⁹ Wengine walidhani kwamba ilikuwa ni upuuzi. “Huyu alikuwa ni Nani, hata hivyo? Mgalilaya tu, Nabii wa bandia,

Mtu ambaye alikuwa ametangazwa ni 'mwendawazimu,' na baraza la makanisa. Mbona," wao walisema, "tunajua ya kwamba Wewe ni mwendawazimu. Una pepo, na utatangazwa 'mtu mwenye kichaa.'" Nalo kusanyiko Lake lilitangazwa kwamba lina "kichaa." Naye mtu aliyemtambulisha, Yohana Mbatizaji, alitangazwa "mshenzi, mwendawazimu kutoka nyikani, mpweke. Mbona, ilikuwa ni bure." Hayo makusanyiko maridadi ya siku hizo hayakuamini ujumbe kama huo. Nazo roho hizo zilizowashikilia kifungoni zinawashikilia mamilioni siku hizi. Wangali hawaamini.

¹³⁰ Lakini kwa wale waliokuwa wakingojea, walijua Bwana wao alikuwa ameahidi kuja kwenye sikukuu. Nao walikuwa wakingojea, wakikusanyika barabarani, na katika vyumba vidogo, na popote walipoweza. Wakizungumza, na kungojea, na mazingira yote yalikuwa yamejawa na kuja Kwake.

¹³¹ Ndivyo ilivyo, siku hizi, Bwana. Wewe uliahidi tutapelekwa kwenye Karamu ya Arusi ya Mwana-Kondoo. Ungekuja kulichukua Kanisa. Nasi tunaona ishara zikitokea, ya kwamba Wewe unakuja, kwa hiyo anga lote limejawa na Kuja Kwako. Tunangojea. Kulikuwako na mikono iliyoinuliwa asubuhi ya leo, Bwana, ya kwamba hawakuwa na hakika bado ya kwamba wangeitwa kwenye Karamu hiyo. Tunakutarajia Wewe uje.

¹³² Wanatwambia wana mabomu yanayoweza kuulipua ulimwengu wote vipande-vipande, katika dakika moja. Wanaweza kuangalia nyota huko Urusi, na kuipimia wakati kabisa kuelekea Louisville, Kentucky, katika dakika moja kamili. Waupige mwezi, na waliubashiria sekunde themanini. Ee Bwana, tunayaona mambo hayo yakitokea kama vile tu Wewe ulivyosema yangekuwa. Nao wanaweza hata na zaidi kutekeleza vitisho vyao.

¹³³ Na, Mungu, tunafungua ukurasa na kuangalia, ya kwamba Wewe unaweza kutekeleza ahadi Yako, kwa kuwa Wewe ni Mungu. Nasi tunakungojea uje. Wachukue watu hawa katika ulinzi Wako, leo hii, Bwana. Wape Uzima wa Milele kupitia kwa Bwana wetu Yesu.

¹³⁴ Jalia, hao walio wagonjwa na wanaotesekeka, wapate kuponywa. Tupe ibada kuu usiku wa leo, katika ibada ya uponyaji inayokuja.

¹³⁵ Wabariki wote, pamoja, katika kila kanisa lililowakilishwa hapa, watu mbalimbali wa awamu mbalimbali za imani. Jalia watambue ya kwamba sio imani ya kanisa wanalohudhuria, inayowafanya kile walicho. Ni imani yao isiyoghoshiwa waliyo nayo katika Mwana wa Mungu. Sifa zote zitakuwa ni Zako, Baba. Tunawakabidhi Kwako, katika Jina la Yesu. Amina.

Yesu alilipa yote. (Hivyo ndivyo alivyofanya.)

Ninii yangu yo- . . . ninawiwa na Yeye;

Dhambi ilikuwa imeacha doa jekundu sana,

Akaiosha ikawa nyeupe kama theluji.

¹³⁶ Sasa ujumbe umekwisha, hebu tumwabuduni tu Bwana, katika kuimba.

Yesu alilipa yote.

Ninawiwa Naye yote;

Dhambi ilikuwa imeacha doa jekundu sana,

Akaiosha ikawa nyeupe kama theluji.

Huko chini msalabani alipofia Mwakozi wangu,

Huko chini nililia nipate kuoshwa kutokana na dhambi;

Loo, hapo Damu ilipakwa moyoni mwangu;

Utukufu kwa Jina Lake!

Utukufu kwa Jina Lake, Jina la thamani!

Utukufu kwa Jina Lake!

Loo, hapo Damu ilipakwa moyoni mwangu;

Utukufu kwa Jina Lake!

¹³⁷ Sasa hebu tusingaliane. Hebu tuangalie juu; tuinue mikono yetu.

Nimeokolewa kutoka dhambini kiajabu,

Yesu anakaa ndani kwa utamu sana,

Pale msalabani ambapo alinichukua;

Utukufu kwa Jina Lake!

Utukufu kwa Jina Lake, Jina lile la thamani!

Utukufu kwa Jina Lake!

Hapo Damu ilipakwa moyoni mwangu;

Utukufu kwa Jina Lake!

¹³⁸ Sasa ninawatakeni mgeuke tu na kupeana mikono na mtu fulani mbele yako, nyuma yako, upande wa kulia na wa kushoto, tunapouimba huu.

Njoo kwenye chemchemi hii tajiri sana na tamu;

Itupe maskini nafsi yako miguuni pa Mwokozi;

Loo, jitumbukize leo, na ufanywe mkami- . . .

Sasa hebu tuinue mikono yetu.

Utukufu kwa Jina Lake!

Utukufu kwa Jina Lake!

Loo, utukufu kwa Jina Lake!

Loo, hapo Damu ilipakwa moyoni mwangu;

Utukufu kwa Jina Lake!

¹³⁹ Linakufanya kujisikia vizuri sana, umesuguliwa kabisa sasa, ukingojea? Loo, ni ajabu jinsi gani!

Njoo kwenye chemchemi hii tajiri sana na tamu;

Itupe maskini nafsi yako miguuni pa Mwokozi;

Loo, jitumbukize leo na ufanywe mkamilfu;
Utukufu kwa Jina Lake!

Utukufu kwa Jina Lake, Jina la thamani!
Utukufu kwa Jina Lake!

Hapo Damu ilipakwa moyoni mwangu;
Utukufu kwa Jina Lake!

Hilo halikufanyii jambo fulani? Wazia hili.

Nimeokolewa kutoka dhambini kiajabu,
Yesu kwa utamu sana huishi;

Kaa! "Mkikaa ndani Yangu, na Neno Langu ndani yenu."

Pale msalabani ambapo alinichukua;
Utukufu kwa ninii Lake. . .

Sasa weka tu nia yako juu Yake, unapomwabudu.

Utukufu kwa ninii Lake. . .

¹⁴⁰ Tungefanya nini, Bwana, bila Wewe?

Utu- . . .

Hii ndiyo saa ya kuonekana Kwako. Wewe unakuja hivi karibuni, Bwana.

Hapo Damu ilipakwa moyoni mwangu;
Utukufu kwa Jina Lake!

¹⁴¹ Loo, jamani! Kuna kitu fulani kuhusu hilo, kinapitia tu ndani yangu mpaka kila mshipa wa mwili wangu unatikisika tu. Huyu ni Roho Mtakatifu hapa. Hum! [Ndugu Jackson ananena kwa lugha nyingine, na kutoa tafsiri—Mh.] Amina. Mungu ashukuriwe. Hayo ndiyo niliyokuwa nikizungumzia.

Imani yangu inakutazamia Wewe,
Ewe Mwana-kondoo wa Kalvari,
Mwokozi wa Kiungu;
Sasa nisikie ninapoomba,
Ondolea mbali dhambi zangu zote,
Loo, nijalie tangu leo
Kuwa Wako kabisa!

¹⁴² Niliuimba huo kwa kusudi fulani. Bwana amenipa somo kwa ajili ya usiku wa leo, kupitia kwa huo ufasiri. "Neno Langu." Mnaona?

Wakati nikitembea katika mzingile mweusi wa maisha,
Na majonzi yanaenea kunizunguka pande zote,
Uwe Kiongozi wangu;
Liamuru giza liwe mchana,
Pangusa hofu, woga wote,
Wala usiniache nitangatange
Kutoka Kwako.

¹⁴³ Miaka miwili iliyopita, katika yale makaburi ya mapangoni huko Saint Angelo, makaburi ya mapangoni huko Rumi, nilikuwa nimesimama kule chini. Nami nikaangalia huko chini, ndipo nikaona mahali walipokuwa wamezichonga picha za hao watakatifu, miaka elfu mbili iliyopita, za Yesu. Moja ya hizo amebeba kondoo aliyepotea mgongoni Mwake; hiyo nyingine akiwaponya wagonjwa na wanaoteseka. Nikasimama pale, huku mikono yangu iko juu namna *hii*, Nikaimba:

Ninapopitia kwenye mzingile mweusi wa
maisha,
Na huzuni zinaenea kunizunguka pande zote,

¹⁴⁴ Ndipo nikaondoka huko, nikaenda kwenye ule uwanja mduara, na kusimama kwenye yale maeneo kule, ambako waliwalisha watakatifu kwa simba. Nao wapiganaji wakawaua. Nikawazia, “Ee Mungu! Imani ya baba zetu, ingali inaishi, inawaka moyoni mwangu! Bwana, kamwe usiiruhusu kuondoka humo. Wala usiniache nitangatange kutoka Kwako.” Hiyo ni kweli. Jinsi ninavyompenda!

Kuna Chemchemi iliyojaa Damu,
Iliyotolewa kwenye mishipa ya Imanueli,
Nao wenye dhambi wakitumbukizwa chini ya
mafuriko hayo,
Hupoteza waa lao lote la hatia.
Hupoteza waa lao lote la hatia,
Hupoteza waa lao lote la hatia;
Nao wenye dhambi wakitumbukizwa chini ya
gharika hilo,
Hupoteza ninii lao lote la hatia . . .

¹⁴⁵ Je, hamna furaha mmefanya hivyo? Sijui kama tunaweza tu kufunga macho yetu. Tuseme:

Mwivi anayekufa alifurahia kuona
Chemichemi hiyo katika siku yake;
Na hapo naomba mimi, ingawa ni mwovu
kama yeye,
Niliusha na kuondolea mbali dhambi zangu
zote.
Niliusha na kuondolea mbali dhambi yangu
yote,
Nioshwe na kuondolea mbali dhambi zangu
zote;
Na hapo naomba mimi, ingawa ni mwovu
kama yeye,
Niliusha na kuondolea mbali dhambi zangu
zote.

¹⁴⁶ Mnajisikia vizuri? Kuabudu tu kwa Roho Mtakatifu, baraka za Bwana juu yenu.

¹⁴⁷ Sasa, tunatarajia kuwaona usiku wa leo. Nazo kadi za maombi zinatolewa sasa saa kumi na mbili u nusu, kamili, ili kwamba hamtaitatiza ibada ifuatayo. Nanyi mnaotaka, njoni.

¹⁴⁸ Basi ni wangapi wanaenda Mbinguni, kwa neema ya Mungu? Hebu tuone mkono wako. Tunapaa juu.

Nina Baba huko ng'ambo,
Nina Baba huko ng'ambo,
Nina Baba huko ng'ambo,
Kwenye ufuko mwingine

Loo, siku moja angavu nitaenda kumwona,
Siku moja angavu nitaenda kumwona,
Siku moja angavu nitaenda kumwona,
Kwenye ufuko mwingine.

Loo, siku hiyo angavu huenda ikawa ni kesho,
Siku hiyo angavu huenda ikawa ni kesho,
Siku hiyo angavu huenda ikawa ni kesho,
Kwenye ufuko mwingine.

Loo, huo si utakuwa ni mkutano wenye furaha!
Huo si utakuwa ni mkutano wenye furaha!
Huo si utakuwa ni mkutano wenye furaha!
Kwenye ufuko mwingine.

¹⁴⁹ Mnazipenda hizo nyimbo za kale? Loo, mnaweza kuchukua nyimbo zenu duni zilizokatwakatwa zote mtakazo. Nipeni hizo nyimbo za kale za moyoni za Damu ambazo hunifanyia kitu fulani humu *ndani*, zilizoandikwa na Roho Mtakatifu, zikaandikwa na Mungu. Hizo ni halisi.

¹⁵⁰ Vema, Bwana awabariki, vizuri sana. Ninatumaini kuwaona usiku wa leo. Nitairudisha ibada kwa mchungaji, sasa, Ndugu Jackson.

[Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . . kawaida.

¹⁵¹ Huenda kukawa na wengine hapa ambao hawawezi kuja kwenye ibada ya uponyaji usiku wa leo, wanataka tu kupakwa mafuta na kuombewa. Kunalo kundi zima letu wahudumu hapa tungefurahi kuwahudumieni kwa njia yoyote tuwezayo. Sasa, ibada ya kawaida ya uponyaji itakuwa ni usiku wa leo. Sasa, hiyo ni, kama unaweza kukaa na kungojea. Kama huwezi, njoo papa hapa sasa.

¹⁵² Kuna mama ambaye hana budi kwenda, huko nyuma, aliye na ugonjwa wa moyo, ama kitu kama hicho. Ninaamini yuko hapa juu. Mtu fulani alielekeza kidole chao hapa juu. Mama hapa aliye na ugonjwa wa moyo, ambaye hawezi kurudi usiku wa leo, aliye mahututi sana, naye anataka . . . wala hawezi kuja mstarini.

¹⁵³ Sasa, mnaona, sababu ya sisi kufanyiza mstari, mle ndani tunaweza . . . Mimi mwenyewe . . . Kila mtu ana njia tofauti ya kuomba. Wengine wanaomba kwa njia moja, wengine nyingine.

Yangu, kama ninajua kile ninachozungumzia, basi ninaweza kutenda.

¹⁵⁴ Lakini kama nilitoka hapa nje, tuseme, nilikuwa nikienda kutengeneza gari, wala sijui neno kulihusu. Vema, ningejichukulia mkebe, na kuuangalia kote. Ni—nisingejua. Mnaona?

¹⁵⁵ Vema, sasa, watu wengi wana hiyo imani ya kutiisha ambayo inatoka moja kwa moja huko nje na kuyapa changamoto mambo hayo na kuyatupilia mbali. Kwangu mimi, sina budi kuona ni nini mpango wa Mungu kwa ajili ya hilo, kwanza, mnaona. Huna budi kuangalia. Karama ya unabii ni kitu cha kigeni. Unaweza kufanya mambo nayo na kujiingiza matatani. Ni wangapi wanaojua hilo?

¹⁵⁶ Mwangalie Eliya, ninaamini ndiye, naam, Eliya. Yeye alikuwa jamaa mdogo, akaingia upara, nao watoto wadogo wakaanza kumdhihaki kuhusu kuwa na upara. Kasema, “Kwa nini hukupaa juu kama Eliya alivyopaa?” Ndipo akageuka na kuweka laana juu ya watoto hao, ndipo arobaini na wawili wao wakauawa. Hiyo siyo tabia ya Roho Mtakatifu. Mnaona? Huyu alikuwa ni nabii huyo, aliyekasirika, naye akaweka tu laana juu ya yale uliyosema.

¹⁵⁷ Yesu alisema, huku chini katika Maandiko ambayo niliyasoma asubuhi ya leo, “Ukiuambia mlima huu, ‘Ng’oka’ wala usione shaka moyoni mwako, bali uamini ya kwamba yale uliyosema yatatimia, yatakuwa yako.” Haya basi. Unaona? Inakupasa kuangalia yale unayofanya.

¹⁵⁸ Sasa, mwangalieni Musa. Yeye alikuwa na nguvu. Hayakuwa ni mapenzi ya Mungu kutoa maji kutoka mwambani (Ni wangapi wanaojua hilo?) mara ya pili. Alipaswa kusema nao, sio kuupiga. Mungu alimwambia asema nao. Akageuka moja kwa moja na kuupiga, maana alikuwa na nguvu za kufanya hivyo. Mungu akampeleka juu mlimani, akasema, “Angalia huko ng’ambo, uitazame ile nchi, bali sitakuruhusu kwenda kule, kwa sababu ya yale uliyofanya kule chini mwambani.” Mnaona? Mnaona?

¹⁵⁹ Kwa hiyo inakubidi kuangalia katika kufanya hivyo. Hiyo ndiyo sababu sikuzote ninajaribu. . .

¹⁶⁰ Nami ninajisikia kwamba hivi karibuni, labda katika siku chache zijazo, ninahisi ya kwamba Mungu atasema nami tena. Mnaona? Ninakaa mwituni, usiku na mchana, nikiungojea wakati huo. Nimekuwa nikihisi, kwa majuma mawili ama matatu yaliyopita, ya kwamba Yeye alikuwa anaenda kungea nami. Ninaamini nitakuwa na badiliko fulani. Nimelitazamia, kwa muda mrefu. Ule, ule ubashiri uliotolewa hapa si muda mrefu uliopita, juu ya yale yangetukia, yalitukia. Lakini inaonekana tu kama, chini ndani yangu, kuna kitu fulani kinachojongea. Nami ninakaa tu huko nje, ninaenda asubuhi na mapema, huko nje usiku, nikingojea, nikiangalia nione yale Yeye

atakayosema. Na kila baada ya kitambo kidogo, nitapiga magoti na kusema, “Uko hapa, Bwana? Kuna jambo lolote unalomtaka mtumishi Wako ajue?” Hiyo ndiyo sababu ninaangalia. Ninataka saa hiyo ije, ambapo haitatubidi kuwa na upambanuzi, ambapo nina imani bila huo.

¹⁶¹ Nafikiri, ono huja hapa, linasema, mwanamke *huyu*, ama mama *huyu*, ama yeyote yule. Mnaona, sijui, mtu, hata uwe nani, atakayekuja hapa juu. “Sijawahi kukuona maishani mwangu.” Na hata hivyo, Yeye ananionyesha pale wewe ni nani, shida yako ni gani, mahali unapotoka, kile ulichofanya kusababisha hili. Hapana budi pawe na chanzo cha kila kitu.

¹⁶² Basi vipi kama mtu fulani alitenda dhambi? Labda kweli walifanya jambo fulani ambalo hukupaswa kufanya. Labda walipaswa kufanya jambo fulani ambalo hawakufanya, ama kitu fulani cha namna hiyo. Nao hawa hapa, huku Mungu akimruhusu Shetani kuishikilia laana hiyo juu yao, kuwaleta kwenye jambo fulani, kwenye—kwenye utiifu. Maradhi wakati mwingine ni kiboko anachotumia Mungu kuleta utiifu. Basi vipi kama mtu huyo akisimama pale, niseme, “Loo, haleluya, utukufu kwa Mungu, Mungu asifiwe,” niwapake mafuta na kuwaombea; ndipo itukie kwamba nimtoe huyo pepo kwao, naye Mungu alimruhusu awekwe pale? Niko matatani, papo hapo, na Mungu. Mnaona ninalomaanisha? Mimi. . .

¹⁶³ Ila ninapoona pale ya kwamba Bwana anasema jambo fulani-fulani. Labda Shetani alilifanya tu. Nami ninaona hakuna kitu katika maisha ya mtu huyo cha kuzuia, basi nina imani ya kwenda pale. Ninayo imani kwa sababu nilimwona Yeye wakati aliposhuka na kuniambia nifanye hivyo. Mnaona?

¹⁶⁴ Halafu basi, jambo lingine ni, labda kama wamefanya jambo baya, nami niseme, “Ulifanya jambo fulani-fulani.”

“Hiyo ni kweli.”

“Vema, sahihisha hilo.”

¹⁶⁵ “Ninaahidi mbele za Mungu nitalisahihisha.” Ninaangalia tena na kuwaona ni wazima, huko ng’ambo, miaka ijayo, wangali ni wazima. Ndipo unajua; Mungu tayari amelinena.

¹⁶⁶ Ananingojea tu niseme neno, hivyo tu. Mnaona? Hilo ndilo linalohitajika. Hiyo ndiyo njia. Ninaangalia, ninaifanya huduma yangu pole pole, ninachukua kila kisa na kukiangalia, ndipo ninajua yale ninayozungumzia. Mnaona? Ninajua la kumwambia mtu huyo hasa.

¹⁶⁷ Sasa, kuna nyakati nimeona mauti juu ya mtu, nisingesema chochote. Ninasema tu, “Bwana akubariki. Mwamini Mungu. Mungu atakuponya, kama ukiwa tu na imani.” Ninaendelea namna hiyo, nikijua, moyoni mwangu, ya kwamba hawataishi. Kwa sababu, vema, kamwe hutaki kuwaambia hivyo,

isipokuwa—isipokuwa ikulazimu kufanya hivyo, iwapo Roho Mtakatifu akilifunua.

¹⁶⁸ Mnajua hilo limefanywa, mara nyingi. Kuwaambia, useme, “Afadhali ujitayarishe. Unaondoka. Hakuna kitu kitakachokuokoa.”

¹⁶⁹ Nilikuwa na msichana mdogo hapa, wakati fulani uliopita, baba yake akasema, endapo msichana huyo mdogo ataponywa, yeye angekuwa Mkristo. Nilitaka familia hiyo iwe ya Kikristo. Nikaenda huko chini nyumbani. Huyo mtoto mdogo alikuwa na nimonia maradufu. Walikuwa wamempa penisilini yote wangaliweza kumpa. Haikufanya chochote. Aliendelea kudhoofika zaidi na zaidi na zaidi. Basi nikashuka kwenda kumwona. Nikaingia mle, na kusema, “Sijui.” Nikasema, “Ni—nitaomba.” Basi nikaingia na kumwombea, na kwa moyo wangu wote.

¹⁷⁰ Ndipo daktari akaja, alasiri hiyo, akasema, “Homa yake imeshuka.” Kesho yake asubuhi akaja, kasema, “Mtoto huyo amepata nafuu sana,” kasema, “anaweza kuamka, kufikia huo usiku.”

¹⁷¹ Loo, baba yake, nilipoenda kumwona, alinilaki, naye alikuwa akishangilia. Akasema, “Loo, Ndugu Branham!”

Nami nikasema, “Lee, nina furaha sana kumwona mtoto wako namna hiyo.”

¹⁷² Ndipo Roho Mtakatifu akanitokea, kasema, “Yeye hataishi ila siku tatu.”

¹⁷³ Naye huyo baba alikuwa amjie Kristo. Kasema, “Sasa, utakapokuwa na mkutano wako, niko tayari kubatizwa,” yeye na familia yake. Sasa, ni—nisingeweza kumwambia. Nilichukia kumwambia. Nilijua mtoto huyo atakufa.

¹⁷⁴ Nikarudi nikamwambia mke wangu, nikawaambia, loo, marafiki wengi sana na jirani zangu, na kadhalika, “Mtoto huyo mchanga hataishi,” msichana mdogo mwenye umri wa kama miaka minane. Nikasema, “Hataishi. Atakufa katika siku tatu.” Nilimwona mama huyo amesimama pale, akilia, akakiinamisha kichwa chake mara tatu, machozi yakatiririka. Nikaona maskini jeneza dogo, jeupe likipitia humo vyumbani, niliposimama pale. Nikasema, “Ataondoka.”

“Vema,” kasema, “unapaswa kwenda kumwambia Lee?”

¹⁷⁵ Nikasema, “Sitaki kumwambia.” Nikasema, “Ninampenda mtoto Beatrice, kwanza, nami...” Ninyi nyote mnajua yule ninayenena habari zake. Kwa hiyo nikasema, “Nampenda mtoto Beatrice, wala si—sitaki ajue hilo. Wala sitaki kumwambia baba yake.” Na—nami nikasema, “Si—sijui la kufanya. Lakini ninajua mtoto huyo mchanga...” Katika siku tatu alikuwa ameaga dunia. Mnaona? Nilisema sikutaka kumwambia baba yake. Mnaona? Sasa, kwa njia hiyo.

¹⁷⁶ Sasa, mara nyingi, nimeenda na kuomba. Katika Afrika kule, ambako kulikuwako na yapata watu watatu tu ama wanne jukwaani. Na wakati jambo fulani lingetukia jukwaani, ningefanya tu maombi ya kusanyiko, ndipo miujiza elfu ishirini na tano ikafanyika mara moja. Mnaona? Ni imani ya watu. Sasa, mara nyingi, tungewaleta watu moja kwa moja jukwaani, tuwawekee mikono, tuwaombee, na kuwaachilia waondoke. Wanaondoka na wanapata afya. Mnaona? Kwa hiyo, ni yoyote yale watu wanayowazia. Ni imani yao, kwa vyovyote vile.

¹⁷⁷ Lakini, kulaani kitu, ninataka kujua kwanza yale ninayofanya. Huyu ni mimi nikilifanya basi.

¹⁷⁸ Ukija, uwekewe mikono, hiyo ni imani yako, hilo ndilo unaloamini. Mnaelewa ninalomaanisha sasa, kila mtu? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Mnaona? Na ninaogopa kusema. . .

¹⁷⁹ Huyu hapa anakuja mtu, sijui lolote kuwahusu, kamwe sijawahi kuwaona awali, "Ndugu Branham, nina *hiki na hiki*. Ni. . . Ni—ni—ni—nina kansa. Nina kifua kikuu."

¹⁸⁰ Ninaogopa tu kusema hivyo. Mnaona, sijui kile ninachofanya. Mnaona? A—afadhali niseme tu, "Nitakuombea." Mnaona, namna hiyo. Lakini ninapoweza kuona ono, nione kile kitakachotukia, hilo ni tofauti. Mnaona? Ni—ninajua la kufanya. Ni—ni—ninafahamu basi, ilicho. Ni kama tu kuingia katika kitu chochote. Lakini mara nyingi ninawaombea watu, mara mia kadhaa.

¹⁸¹ Ndugu Scharrer aliyeketi papo hapo nyuma, ninamwangalia sasa. Nilikuwa mahali fulani kwenye ibada ya mazishi, nikamzika mama ya Dada Roberson. Ndugu Scharrer, sijawahi kumwona mtu katika hali yoyote zaidi, kuliko aliyokuwa nayo, mimi. . . kuumwa na kichwa kipandauso, ama chochote kile. Sijui. Basi akafikia mahali akapoteza fahamu, hakujua chochote. Nikaingia moja kwa moja chumbani mwake, nikaomba tu maombi mafupi, nikatoka nje. Nikasema, "Kwa hakika kadiri ninavyosimama hapa, yeye ataponywa." Na hilo lilikuwa ndilo. Nikatoka moja kwa moja nje.

¹⁸² Bibi Wood pale, mama yake amelala, akifa kwa kansa usoni mwake. Mnajua ni kitu gani. Hata ukigusa mdomo wako hapa, humu *ndani*, unaweza kufa katika muda mfupi. Nyuki alimchoma mtu, hapa chini ya New Albany, hivi majuzi, akamchoma mdomoni, akafa katika yapata dakika mbili. Chochote mahali *hapa*, kamwe usibinye chochote midomoni mwako, maana inaingia kwenye mshipa unaoingia ubongoni mwako. Kweli, watu, mtu kamwe hapaswi kunyoa nywele midomoni mwao. Hiyo ni kweli kabisa. Wakati wembe wako unapovuta, machozi yanaingia machoni mwako. Ni pabaya papo hapo ndani, kwenye mshipa mkuu.

¹⁸³ Hapa wakati fulani uliopita, nilikuwa hapa ambapo Gene na Leo. . . Palikuwapo na msichana pale, aliyefanya kazi kwenye duka la dawa, hapa—hapa chini kwenye duka la dawa. Nami nikaingia mle ndani kununua namna fulani ya kitu fulani kwa ajili ya watoto wangu, kununua vitamini, na kadhalika kwa ajili ya mafua yao, na kadhalika. Naye alikuwa akilitangaza kule kwenye ujirani.

¹⁸⁴ Kulikuwako na mhudumu fulani pale. Akasema, “Unataka kuniambia ya kwamba Ndugu Branham angempa mmoja wa watoto wake dawa?” Mnaona, haijulikani. Nami nikasema. . . “Vema,” akasema, “sina imani naye tena hata kidogo.” Ndipo siku mbili tu baada ya hapo, yeye alikuwa akinyoa, akakata mdomo wake, akaubinya namna *hiyo*. Alikuwa hospitalini, kesho yake, chini ya kihema cha oksijeni. Yapata siku nne ama tano baadaye, akatoka, uso wake ukavimba namna *hiyo*. Mnaona? Ukaja namna *hiyo*, maana alibinya mahali fulani mdomoni mwake. Mnaona? Inakubidi kuwa mwangalifu kuhusu yale ufanyayo kuhusu hilo, hilo tatizo la mdomo *humu* ndani.

¹⁸⁵ Sasa, turudi kwenye roho, upande wa kiroho. Mnaona? Inakupasa kujua kile unachokaribia, kile unachofanya. Ikiwa hujui, usifanye hivyo.

¹⁸⁶ Sasa, katika maombi kwa ajili ya wagonjwa, loo, ningeweza kusema mambo mengi, mengi sana. Bibi Wood, niliyekuwa nikinena habari zake, mama yake, kansa ilikuwa imeingia katika mishipa hii hapa. Uso wake ulikuwa umevimba. Mimi, Leo, pamoja na Gene tulikuwa Michigan. Nasi tukasikia hilo kwenye simu. Mke wangu alinipigia simu, kasema, “Mama ya Bibi Wood yuafa.”

¹⁸⁷ Nikavuka mto. Huyo hapo Bibi Wood ameketi, amechanganyikiwa kabisa. Alisema mama yake yuafa. Nikaingia chumbani, na kukaa mle pamoja naye muda mrefu, bila ono. Lakini wakati tu nilipomwendea, kitu tu ndani yangu, kikasema, “Yeye ataishi.” Nikarudi nje.

¹⁸⁸ Bw. na Bibi Wood wanaoketi pale, kasema, “Vema, Bwana alisema nini? Uiona ono?”

¹⁸⁹ Nikasema, “La.” Wao. . . upesi sana. Waliishakuwa mkutanoni, mnaona, na kuyaona hayo maono. Walikuwa wamehuzunika. Lakini katika dakika moja tu, nikasema, “Lakini kitu fulani kiliniambia. Ni BWANA ASEMA HIVI tu kama vile ono, kwamba mwanamke huyo ataishi.” Naye akaishi.

¹⁹⁰ Kansa *hapa*, chini usoni mwake namna *hiyo*. Nayo hapa tayari imeingia kwenye mfupa, ikaula mfupa kabisa, na kadhalika kote namna *hiyo*, nyama yote kuingia kwenye mfupa namna *hiyo*. Naye anaishi leo hii, hakuna hata angalau kovu pale mahali ilipokuwa. Mnaona? Na kile kilichoitawanya, daktari alikuwa amemdungu sindano, nayo ikaitawanya kote, mnaona.

Naye huyo—huyo alifanya, ama alijaribu kuichoma, ama kitu fulani wanachojaribu kuifanyia.

¹⁹¹ Sasa, ni imani ya hao watu, mahali imani yako ilipo. “Kama ukininii. . .” Hapa, Yairo alisema, “Njoo ukaweke mikono yako juu ya msichana wangu, binti yangu, naye ataishi.” Mnakumbuka hilo?

¹⁹² Yule Mrumi alisema, “Sistahili Wewe kuja chini ya paa langu. Sema tu neno, naye mtumishi wangu ataishi.” Hiyo ni kweli? Haya basi. Inategemea imani.

¹⁹³ Sasa, huyo mama yuko hapa aliye na ugonjwa wa moyo, asiyeweza kurudi usiku wa leo? Ikiwa yuko hapa. . . [Ndugu Jackson anasema, “Hapa nyuma, upande wa kushoto hapa.”—Mh.] Upande wa kushoto. Vema, bwana. Vema, msichana, kama unataka kuja moja kwa moja huku sasa, njoo tu moja kwa moja.

Mtu mwingine yeyote? Umekaribishwa.

¹⁹⁴ Ninamtaka Ndugu Cash, na ndugu. . . ninyi ndugu hapa. Ninaamini Ndugu Beeler yuko miongoni, pia, sivyo? Njoo hapa, Ndugu Beeler. Mhubiri mwingine, yeyote wa wahudumu ambao wangetaka kuja sasa, tunataka kumwomba msichana huyu.

¹⁹⁵ Walisema ulikuwa ni ugonjwa wa moyo. Sivyo? Huo ndio mwuaji mkubwa sana tuliye naye, ugonjwa wa moyo. Lakini unajua ya kwamba Yesu anaishi moyoni? Umemkubali mle ndani? Wewe, loo, unaishi hapa mjini, sivyo? [Dada huyo anasema, “Kutoka Ohio.”—Mh.] Ohio. Unaweza kuponywa ugonjwa wako wa moyo. Mungu ndiye mponyaji. Yeye huponya moyo. Huponya kila kiungo cha mwili, kila ogani.

¹⁹⁶ Sasa njoni *huku*, ndugu. Hebu tuje mahali huyu mama alipo.

¹⁹⁷ Ninalitaka kusanyiko kuinamisha kichwa chao, tafadhalini, wakati tukiomba, . . . ? . . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

¹⁹⁸ Wewe huufanya moyo. Unaufanya kukua na kuishi. Unaweza kujenga ukuta mpya ambapo ule wa kale umebomolewa. Kwa kuwa Wewe ni Mungu, na Mungu peke yake. Nami nawazia, “Vipi kama huyu alikuwa ni dada yangu, Delores; mke wangu, Meda; ama msichana wangu, Rebekah?” Ningelitaka kanisa liombe kwa yote yaliyo ndani yetu, Bwana, kuomba ombi la imani kwa mtoto wangu, ama mke wangu, ama mpendwa. Labda ni binti ya mtu fulani, na labda mke wa mtu fulani. Huenda ikawa ni mama ya mtoto fulani. Yeye alisema alikupenda, naye amekukubali Wewe kama Mwokozi wake. Naye anazo haki za kuja kwenye majaliwa haya. Nasi tunakuja, juu ya mamlaka ya mwaliko Wako, kumhudumia, karama hizi za uponyaji. Na kwa kuweka mikono juu yake, jalia Neno la Mungu lidhihirishwe mwilini mwake, kuiondoa shida hii ya moyo.

¹⁹⁹ Tunailaani, juu ya msingi wa Neno la Yesu Kristo mwenyewe, likisema, ya kwamba, “Maombi ya imani yatamwokoza mgonjwa huyo, naye Mungu atawainua.” Sasa,

katika Jina la Yesu Kristo, jalia hiyo shida ya moyo imwache dada yetu. Jalia aende, pasipo na wakati mmoja kuweco na doa lake tena. Nawe utapata sifa na utukufu kwa ajili ya baraka hizi, ambazo zinaweza tu kuja kwa mkono Wako, tunapohudumu kulingana na Neno Lako. Amina. Mguse, Bwana.

Kuwa na imani na uliamini, dada! . . . ? . . .

²⁰⁰ Mungu mpendwa, maskini mikono hii dhaifu, yenye makunyanzi ya mama huyu mpendwa, imewahudumia watoto wake, na kwa wajukuu wake, na imenihudumia mimi mara nyingi, naye ni mhitaji asubuhi ya leo. Nasi tunasimama, baada ya kuhubiri ya kwamba Wewe ni Mungu mkuu sana, Mungu mkuu sana, mwenye nguvu, wala sio Mungu wa historia; Mungu wa wakati uliopo, "MIMI NIKO." Nami naomba, Ee Bwana Mungu, ya kwamba utatuma baraka Zako za uponyaji juu ya mwili wake. Mikono juu yake, katika Jina la Yesu. Jalia aondoke hapa leo hii, na apate afya, na kuishi miaka mingi yenye furaha bado, kukutumikia Wewe. Nawe utapata sifa zote kwa ajili ya mambo haya, wakati akitembea na kuwaambia watu yale ambayo yametukia. Amina.

²⁰¹ Haleluya! Marion Williamson, Mungu akubariki. Nyote wawili mlinipigia simu. Nikazungumza nanyi . . . ? . . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

²⁰² Naam. Nilimwombea, miaka kadhaa iliyopita, akiwa na kifua kikuu. Akaponywa. Yeye ni mgonjwa, lakini hana budi kupata utambuzi, kujua ni nini hasa . . . yale aliyofanya, ama chochote kulihusu. Ambalo ninaamini, hata hivyo, ya kwamba msichana huyu na hao wengine tuliowaombea, muda mfupi uliopita, watapata afya. Ninaamini hayo kwa yote yaliyo ndani yangu. Ninaamini tu. Mnaamini pia? Nina hisia ya namna ile ile kuwahusu ambayo nilikuwa nayo kuhusu mama yako, Bibi Wood, unaona; ama kama nilivyokuwa nayo kwako, Ndugu Scharrer; na wengine wengi hapa. Ninahisi tu kwamba wataponywa. Hivyo tu. Wao—wao wame—wao wameendesha gari mbali sana wakaja kwenye ibada, na hiyo inaonyesha imani yao.

²⁰³ Mnajua, Biblia inanena juu ya hilo, katika siku za mwisho? Hiyo ni kweli. Loo! "Itakuwa Nuru wakati wa jioni." Hiyo ni kweli? Itakuwa Nuru, Injili ile ile. Roho Mtakatifu yule yule, Nguvu zile zile za Mungu zingekuwa hapa kuwaponya wagonjwa na wanaoteseka, kama alivyokuwa. Naye Mungu yupo sasa hivi, yupo sasa hivi. Yeye yupo tu sasa kama vile atakavyokuwa usiku wa leo, yule yule tu, kuwaponya wagonjwa na wanaoteseka. Yeye si ni mwema?

²⁰⁴ Hebu tuimbe wimbo, huu, "Wa ajabu, Yesu kwangu." Dada, unaujua huo?

Wa ajabu, wa ajabu, Yesu kwangu,

Yeye ni Mshauri, Mfalme wa Amani, Mungu
Mwenye Nguvu.

Hebu tuuimbe sasa, pamoja.

Wa ajabu, wa ajabu, Yesu kwangu,
Yeye ni Mshauri, Mfalme wa Amani, Mungu
Mwenye Nguvu;

Loo, huniokoa, hunilinda na dhambi zote na
aibu,

Wa ajabu ni Mkombozi wangu, Jina Lake
lisifiwe!

Loo, wa ajabu, wa ajabu, Yesu kwangu,
Yeye ni Mshauri, Mfalme wa Amani, Mungu
Mwenye Nguvu;

Loo, kwa kuniokoa, kwa kunilinda na dhambi
zote na aibu,

Wa ajabu ni Mkombozi wangu, Jina Lake
lisifiwe!

Wakati mmoja nilikuwa nimepotea, sasa
nimepatikana, huru na hukumu,

Yesu hutoa uhuru na wokovu mkamilifu;

Huniokoa, hunilinda na dhambi zote na aibu,

Wa ajabu ni Mkombozi wangu, Jina Lake
lisifiwe!

Wa ajabu, wa ajabu, Ye- . . .

Uimbeni, kila mtu sasa. Inueni.

Yeye ni Mshauri, Mfalme wa Amani, Mungu
Mwenye Nguvu;

Loo, kwa kuniokoa, hunilinda na dhambi zote
na aibu,

Wa ajabu ni Mkombozi wangu, Jina Lake
lisifiwe!

Loo, wa ajabu, wa ajabu . . .

Inueni mikono yenu wakati . . .

. . . kwangu,

Yeye ni Mshauri, Mfalme wa Amani, Mungu
Mwenye Nguvu;

Loo, kwa kuniokoa, kunilinda na dhambi zote
na aibu,

Wa ajabu ni Mkombozi wangu, Jina Lake
lisifiwe!

²⁰⁵ Amina. Hebu tuinue tu mikono yetu sasa, na kumshukuru,
kila mmoja, katika njia yako mwenyewe.

²⁰⁶ Bwana, tunakushukuru kwa wema Wako. Tunakushukuru
kwa rehema Zako, kwa yote ambayo umetufanyia. Imekuwa ni
vema kuwa hapa. Tunge sema pamoja na Petro na hao wengine,

“Na tujenge vibanda vitatu, kimoja Chako, kimoja cha Musa, na kimoja cha Eliya,” lakini Sauti hiyo iliyobarikiwa inasema, “Huyu ni Mwanangu mpendwa, msikieni Yeye.” Kwa hiyo, Yesu ni wa ajabu, “Mshauri, Mfalme wa Amani, Mungu Mwenye Nguvu, Baba wa Milele.”

²⁰⁷ Kuwa pamoja nasi kupitia siku ijayo, Bwana. Tubariki sasa. Tupe ibada kuu usiku wa leo.

²⁰⁸ Wabariki watumishi Wako kila mahali kote ulimwenguni. Bariki mikutano inayokuja, kote nchini, Bwana, huko San Jose, California, mahali pengine ambapo mikutano na watu wamekusanyika sasa kwa ajili ya ibada kuu. Kuwa pamoja nasi usiku wa leo. Kuwa pamoja na wale jamaa kule maskanini. Kote nchini, kila mahali panapoitwa kwa Jina Lako, jalia, Bwana, ya kwamba utakuwa kule. Katika Jina la Yesu.

²⁰⁹ Sasa nitairudisha ibada kwa mchungaji, ambaye ataturuhusu kuondoka, Ndugu Jackson. Saa kumi na mbili u nusu, sasa, kadi za maombi.

²¹⁰ [Ndugu Jackson anasema, “Ningetaka kusema, ya kwamba tunataka kuchukua matoleo ya upendo kwa ajili ya ndugu yetu leo hii.”—Mh.]

²¹¹ Asante, Ndugu yangu Junior, mpendwa. Asante, hapana kabisa. La. Msifanye hivyo. Msifanye hivyo. Ninajisikia duni sana. Ninajisikia vizuri sana sasa; hamtaki nijisikie vinginevyo, sivyo? Kwa hivyo asanteni, vivyo hivyo tu. Alikuwa anatania tu, aone kile ningesema. Endelea. 

59-1004M Ni Nani Huyu?
Faith Assembly
Clarksville, Indiana Marekani

SWAHILI

©2022 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org